SUPA JACKPOT
TZS. 1,161,795,478
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Alhamisi Oktoba 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581461
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi

TISHIO LA KIHARUSI

## Muhimbili yapata suluhu tiba yake

- **Yasimika** mtambo wa kisasa; unatibu pia saratani, homa ya ini, uvimbe katika kizazi...*Endelea ukurasa 2*



Umati wa abiria ukiwa kwenye adha ya kusubiri usafiri katika stendi ya Kimara Mwisho ya mabasi ya mwendokasi, Dar es Salaam jana asubuhi, huku mabasi saba yakiwa yameegeshwa pembeni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

RIPOTI YA UCHUNGUZI

### Wananchi walivyo hatarini mradi tata wa dhahabu Chunya

UKURASA 4

UKURASA WA 3

**Serikali** yatangaza kasi kushughulikia tatizo la umeme



UKURASA WA 19

**Israel** yazidi kuteketeza Ukanda Gaza

UKURASA WA 3

**Malipo** mafao wastaafu bado mtihani mgumu kwa serikali

### Ziara Samia India yaibua neema soko la mbaazi fursa uwekezaji UK.2

**MICHEZO** MABAO 89 YATINGA NYAVUNI LIGI BARA UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza katika dhifa ya kitaifa iliyoandaliwa na Rais wa India, Droupadi Murmu, Ikulu ya India jana. **PICHA: IKULU**

# Muhimbili yapata suluhisho tishio kiharusi

**Na Beatrice Shayo**

WAKATI ugonjwa wa kiharusi ukiendelea kuwa tishio nchini kwa kusababisha vifo, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), imenunua mtambo wa kisasa wa kutibu maradhi kwenye mishipa ya damu pamoja na ugonjwa huo.

Mtambo huo wenye thamani ya Shilingi bilioni mbili umeshasimikwa kwenye hospitali hiyo na umeanza kutoa huduma rasmi Julai, mwaka huu kwa magonjwa mbalimbali yakiwamo ya saratani, uvimbe kwenye kizazi na homa ya manjano.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, akizungumza na Nipashe jana, alisema mpaka sasa wameshatoa huduma kwa wagonjwa 1,200.

Alifafanua kuwa kati ya wagonjwa hao wamo waliokuwa na matatizo ya mishipa kuziba, homa ya manjano kwa sababu kwenye ini kumeziba, waliovimba miguu kutokana na kuziba kwa mshipa na wenye uvimbe katika mfuko wa uzazi.

Alisema mtambo huo kazi yake kubwa ni kutibu maradhi yoyote yaliyokuwa katika mishipa ya damu, lakini hadi sasa bado hawataanza kutoa matibabu kwa ugonjwa wa kiharusi.

"Wagonjwa wa kiharusi bado hatujaanza kuwafanyia kwa sababu wataalamu wetu wapo kwenye mafunzo ifikapo Novemba na Desemba, mwaka huu, tutakuwa na timu kutoka nchini Marekani.

"Endapo katika kipindi hicho atatokea mgonjwa, tutafanya pamoja na wataalamu hao wa Marekani, lakini matibabu haya kwa ugonjwa wa kiharusi ni wale wanaougua ndani ya saa 24 na awe amefikishwa hospitali mapema," alisema.

Alisema wanapokea simu za watu waliopata kiharusi kwa muda mrefu, lakini mtambo huo hauwezi kuwatibia wagonjwa ambao walipata kiharusi cha muda kirefu.

"Tunapigiwa simu na mtu ambaye amepata kiharusi mwaka jana, hii hapana ukishapita huo muda haiwezekani hata wagonjwa waliopata mshtuko wa moyo kama hajafika hospitali katika zile dakika 90 (saa moja na nusu), hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kufanywa sio Jakaya tu mahali popote duniani," alifafanua.

Akiuelezea mtambo huo, Prof. Janabi alisema pia, unatoa matibabu kwa wagonjwa wenye saratani ya ini kwa mtaalamu kuutumia kupeleka dawa kwenye ini kupitia mishipa ya damu.

Pia alisema mtambo huo una uwezo wa kuyeyusha uvimbe uliopo kwenye mfuko wa kizazi.

Alisema mashine hizo kwa Tanzania zipo mbili; Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) inayofanya kazi ya upasuaji bila kupasua kichwa na Taasisi ya Moyo (JKCI).

"Sisi tunafanya huduma nilizozitaja kwa magonjwa ya mishipa ya damu na ndiyo maana umeona katika kipindi cha miezi mitatu tumewafanyia wagonjwa 1,200," alisema.

Kadhalika, alisema asilimia 85 wanaotoa huduma hizo zinafanywa na wataalamu wa ndani ambao wanajulikana kwa jina la kitaalamu 'intervention radiologist'.

**HALI DUNIANI**

Takwimu zilizotolewa wakati wa Siku ya Kiharusi Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka Oktoba 29, zilionyesha kuwa kiharusi ni ugonjwa ambao umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka duniani huku nchi zenye kipato cha chini na cha kati zikikumbwa zaidi na tatizo hilo.

Ilibainishwa kuwa katika miaka 17 iliyopita, kiharusi kilikuwa kikiongoza kwa kusababisha watu kupata ulemavu. Pia umekuwa ugonjwa ambao unachochea kasi ya vifo huku sababu kubwa zikitajwa kuwa shinikizo la damu, kisukari, unene kupita kiasi, uvutaji sigara, unywaji wa pombe kupitiliza, kutofanya mazoezi na ulaji bila mpangilio.

"Mtu mmoja kati ya wanne yuko katika hatari ya kupata kiharusi. Mwaka 1990 hadi 2019, ongezeko la watu wanaougua kiharusi lilikuwa asilimia 70 huku vifo vinavyotokana na kiharusi vikiongezeka kwa asilimia 43," ilibainisha taarifa hiyo.

Kwa Afrika, ilielezwa kuwa watu 316 kati ya 100,000 walikuwa wakipatwa na kiharusi huku Tanzania watu 95 kati ya 100,000 maeneo ya vijijini wakipatwa na maradhi hayo na mijini ni wastani wa watu 260 kati ya 100,000.

# Ziara Samia India yaibua neema soko la mbaazi fursa uwekezaji

**Na Romana Mallya**

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini India imeibua neema na fursa zaidi za kiuchumi na kibiashara ikiwamo kupatikana kwa soko la mbaazi kutoka Tanzania.

Kutokana na fursa hiyo, Tanzania sasa imepata nafasi ya kuuza wastani wa tani 200,000 kwa mwaka ambazo zitawanufaisha wakulima wa zao hilo ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakililia ukosefu wa soko, hivyo kupata hasara.

Mbali na fursa hiyo ya soko, Rais pia amehamasisha wawekezaji wa India kuwekeza nchini huku akiwaahidi mazingira rafiki ya biashara na mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea.

Samia alitoa ahadi hiyo wakati akihutubia katika Mkutano wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Tanzania na India unaofanyika jijini New Delhi, India ikiwa ni siku ya pili ya ziara yake ya kiserikali ya siku tatu iliyomalizika jana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Rais Samia aliwaeleza wawekezaji hao kuwa Tanzania inatekeleza mageuzi makubwa ya kiuchumi barani Afrika yenye malengo makubwa ya kimaendeleo kwa kutumia sekta binafsi na uwekezaji kama chachu ya ukuaji wa uchumi.

Rais Samia alisema kama sehemu ya mageuzi makubwa, Tanzania imetumia ufumbuzi wa kiteknolojia unaoruhusu wawekezaji wa kigeni kusajili biashara zao na kupokea vibali vya vivutio vya uwekezaji mtandaoni kabla ya kuwasili kwao.

Kadhalika alisema Tanzania imeboresha kanuni zake za biashara hivyo kuwarahisishia wawekezaji.

"Tumehama kutoka kusajili dola bilioni mbili za fedha za miradi ya uwekezaji kutoka Nje (FDI) mwaka 2020 hadi dola bilioni tano katika mwaka unaoishia Juni, 2023. Tunalenga kufikia dola bilioni 15 kwa mwaka ifikapo mwisho wa mwaka 2025," alisema.

Rais Samia, alisema tangu mwaka 1997 hadi sasa, Tanzania imefikia kiwango cha uwekezaji wa zaidi ya dola bilioni 3.87 kutoka India ikiwa na jumla ya miradi 675 na zaidi ya ajira 61,000 zilizotolewa. Alisema hiyo imeifanya India kuwa moja ya wawekezaji watano bora nchini Tanzania.

Pia, alisema mashirika ya kukuza uwekezaji Tanzania Bara na Zanzibar yanalenga kuvutia angalau dola bilioni tatu za uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) kutoka India kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

Aliwaeleza wawekezaji hao kuwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kuwa zimeanzisha dawati maalum kwa ajili ya India lenye wafanyakazi makini kwa ajili ya kutoa kipaumbele na kusaidia wawekezaji kutoka India.

Wakati huohuo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema serikali itajadiliana na India kuhusu suala la biashara ya uhakika ya mbaazi kwa wakulima wa Tanzania na jana Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa habari njema.

Bashe alisema Tanzania imeishawishi na kukubaliwa na India kuiuzia mbaazi kwa wastani wa tani 200,000 kwa mwaka katika kipindi cha miaka miwili hadi mitatu ijayo.

"Ingawa India ni wateja wakubwa wa mbaazi, soko lilikuwa halitabiriki kwa kupanda na kushuka, lakini kwa makubaliano haya, wakulima wa mbaazi watakuwa na uhakika wa soko.

"Kwa sasa, bei ya mbaazi ni wastani wa dola moja ya Marekani kwa kilo. Kwa bei hiyo, hapa tunaongelea biashara ya thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 450 kwa mwaka," alisema Bashe.

Eneo lingine la kilimo ambalo Bashe alisema Tanzania itanufaika ni lile la matrekta ya kilimo baada ya kampuni ya Mahindra kukubali kujenga kiwanda kitakachokuwa na uwezo wa kutengeneza mpaka matrekta 2,000 kwa mwaka.

Bashe alisema tayari upembuzi yakinifu wa jambo hilo umeanza na kwamba kama Mahindra watashindwa, kuna kampuni nyingine iko tayari kufanya kazi hiyo.

Alitaja mafanikio mengine kwenye sekta ya kilimo kutokana na ziara hiyo kuwa yako katika zao la korosho ambapo uamuzi muhimu umefanyika.

"India ina sheria inayotoza kodi ya asilimia 35 kwa korosho ghafi inayoingia kwao. Sasa kuna kiwanda tumefungua cha kubangua korosho na tumekubaliana ile itakayotoka kwenye kiwanja hicho haitakuwa inatozwa kodi hiyo," alisema.

Katika sekta ya afya, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, John Jingu, alisema serikali hizo zimekubaliana kufungua kituo cha huduma za kibingwa za upandikizaji wa figo na ini hapa nchini.

## Wazee walia kutumiwa bila manufaa kiuchumi

**Na Beatrice Moses**

WAZEE wamelalamikia kutumiwa kama vitega uchumi, kufanyiwa ukatili na kutopata huduma bora za matibabu hasa kutopewa dawa kwa wanaotumia kadi za bima.

Katibu wa Baraza la Wazee Kigamboni, Veronica Nyande, aliyasema hayo jana kwenye hafla ya Maadhimisho ya Siku ya Wazee Wilaya ya Kigamboni. Mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Halima Bulembo.

Alisema wanapokwenda katika vituo vya afya kwa kutumia kadi za bima ya afya iliyoboreshwa (iCHF) hawapewi huduma bora huku wakiambiwa hakuna dawa.

"Kuna baadhi ya wanandugu na watoto wanawanyanyasa wazee wao wakishastaafu na wengine wanawapokonya mafao yao na kuwatelekeza," alisema.

Pia alibainisha kuwa kuna wengine wakiwatumikisha wazee kwa kuwafanya ombaomba hatua ambayo huwadhalilisha, hivyo kuiomba, hivyo kuiomba serikali na wadau kutoa elimu kwa jamii ili itambue umuhimu wa kutunza wazee, kupunguza changamoto wanazokabiliana nazo.

Nyande pia aliiomba serikali kutoa ruzuku ya kujikimu wazee kama ilivyo Zanzibar na kufutiwa nauli ya kivuko kwa wazee ambayo inalipwa Sh. 200 kwa safari moja.

Meneja Mwandamizi wa Taasisi ya Health Promotion Tanzania (HDT), Agnes Kisala, ambayo ni wadau wa afya, alisema wamefanikiwa kuwalipia bima wazee 150 kutoka kati ya 4,893 na bado wanaendelea na juhudi za kuwasaidia wengine.

"Tunatoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kuwasaidia wazee wanashindwa kumudu gharama za matibabu, hawa ni hazina njema tuwatunze," alisema.

Dk. Nasri Mangara wa Hospitali ya Kibada ambaye alikuwa miongoni mwa wanaotoa tiba bure kwa wazee waliofika kwenye maadhimisho hayo, alisema wengi wanakabiliwa na tatizo la uoni hafifu lakini hawana fedha za kununua miwani.

"Kuna magonjwa kadhaa yanayowasumbua wazee yakiwamo sukari, presha ya kupanda na vidonda vya tumbo pia macho tunagundua wanatakiwa kuvaa miwani lakini hawawezi gharama za miwani," alisema.

Dk. Mangara alishauri kuwa ni vyema kukawekwa punguzo maalum la miwani pia wadau wachangie wazee waweze kupata kuliko kuwapima bure na kushindwa kuwapa suluhisho la tatizo linalowakabili.

Mzee Remmy Mathaula alisema maadhimisho hayo ni mazuri kwa kuwa wanapata fursa ya kutibiwa bure, lakini walikalishwa muda mrefu kumsubiri mgeni rasmi tangu saa 2:00 asubuhi lakini alifika saa 6:30.

# Malipo mafao wastaafu bado mtihani mgumu kwa serikali

**Na Cynthia mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema ameendelea kupokea malalamiko ya kucheleweshewa mafao watumishi waliostaafu licha ya suala hilo kukemewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Vilevile, ameagiza wakuu wa idara za utawala na rasilimaliwatu katika utumishi wa umma kuzingatia maadili ya kazi zao na kujiepusha na vitendo visivyo vya kiuadilifu kitendaji.

Vitendo hivyo ni pamoja na kutumia vibaya madaraka kwa kufanya upendeleo kwa marafiki, ndugu, jamaa na kughushi nyaraka na wizi.

Jijini Arusha jana wakati akifungua kikao kazi cha wakuu wa idara za utawala na rasilimaliwatu katika utumishi wa umma, Waziri Simbachawene alisema hali hiyo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutowasilishwa michango na tozo, uwasilishwaji wa nyaraka pungufu, wastaafu kuwa na barua mbili tofauti za kupandishwa cheo.

"Ninawaagiza kuhakikisha michango ya watumishi inawasilishwa kwenye mifuko ya hifadhi za jamii kwa wakati na nyaraka zote zinazohitajika zinaandaliwa mapema na hapa ninyi ndio wahusika wakuu, hakikisheni mnafanya kazi yenu.

"Pia yapo malalamiko yanayohusu kuwapo matumizi ya lugha mbaya kwa baadhi ya watumishi wastaafu wanapofuatilia haki zao za nauli, gharama za kusafirisha mizigo baada ya kustaafu, acheni kuwafanyia hivi, sababu leo ni wao na wewe ukistaafu utafanyiwa hivyohivyo," alisema.

Vilevile, waziri huyo alisema kuna tatizo la baadhi ya waajiri kutotenga fedha kwa ajili ya kugharamia stahiki, huku wakifahamu kustaafu si jambo la ghafla, hivyo aliwaelekeza waajiri kushirikiana na wasimamizi wa masuala ya utawala na rasilimaliwatu kuhakikisha wanashughulikia stahiki za watumishi hao kwa wakati.

Maeneo mengine aliyowaonya ni ya matumizi mabaya ya rasilimali za ofisi za umma, vitendo vya udanganyifu, matumizi binafsi ya muda wa kazi, vitendo vya ubaguzi na unyanyasaji kijinsia na matumizi mabaya ya madaraka kwa manufaa binafsi.

"Hali hii ikiendelea kushika kasi kwa kuwa pamoja na dhamana mliyokabidhiwa, mlio wengi hamchukui hatua stahiki za kinidhamu, kwa watumishi walio chini yenu, kazi kubwa mnayoifanya sasa ni kukaa kimya kwa kujifanya hamwoni au kuomba Ofisi ya Rais (Utumishi) kuhamisha mtumishi husika, hali hii haikubaliki, anzeni kuchukua hatua.

"Haipendezi pale mnaposikia viongozi wa ngazi ya kitaifa wanapofanya ziara zao za kikazi, wanatekeleza majukumu yenu. Tumieni fursa hii kujitathmini, mtumishi anayeharibu achukuliwe hatua za kinidhamu mahali alipo na si kukimbilia kumhamisha," aliagiza.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amemulika dosari ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutowasilisha michango ya watumishi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22, CAG Charles Kichere anazitaja Halmashauri za Dodoma Jiji na Nzega kuongoza kwa kutowasilisha kiasi kikubwa cha fedha, Dodoma Jiji ikitakiwa kuwasilisha Sh. bilioni 56.81 zilizotokana na faini.

Simbachawene pia aliwapongeza kwa mafanikio katika nyanja za kiuchumi na kijamii, serikali inajivunia huduma bora zinazotolewa na watumishi wa umma zikiwamo za ujenzi wa miundombinu, ambayo imesanifiwa na ujenzi wake kusimamiwa na watumishi hao.

Pia, aliwasisitiza kusimamaia matumizi sahihi na yenye tija ya mifumo ya kielektroniki iliyoanzishwa na itakayoendelea kuanzishwa na kuwasaidia watumishi walio chini yao kuitumia.

Kwa mujibu wa Simbachawene, suala la kukaimu nafasi za uongozi na ujazaji nafasi lina changamoto nyingi ambazo ni pamoja na maofisa kukaimishwa nafasi hizo kwa muda mrefu pasipo kuanisha mchakato wa ujazaji nafasi hizo na kutoteuliwa watumishi ambao mchakato wao wa uteuzi umekamilika, kuchelewa kuwaombea vibali vya kukaimu na kulipwa posho ya kukaimu na kusababisha ongezeko la madeni serikalini.

Changamoto nyingine ni baadhi yao kuwasilisha maombi yenye nyaraka pungufu hivyo kuchelewesha mchakato wa uandaaji vibali na kuwasilisha orodha ya majina ya maofisa wasio na sifa zinazohitajika kufikiriwa kukaimu au kuteuliwa nafasi za uongozi.

"Kupitia hili naelekeza kila mmoja wenu kufanyia kazi changamoto zote zilizobainishwa kwenye eneo hili na kuanzia sasa ofisi yangu haitoshughulikia maombi yoyote yasiyokidhi vigezo na hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya waajiri na wakuu wa idara za utawala na usimamizi wa rasilimaliwatu kwa kuzingatia mamlaka zao za kinidhamu," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, alisema kikao kazi hicho kinalenga kufanya tathmini ya nafasi ya msimamizi wa rasilimaliwatu na utawala na watajikita katika namna ya kutatua changamoto wanazokabiliana katika utekelezaji majukumu yao na kutafuta namna bora ya kuzitatua ili kuimarisha utendaji kazi na kuleta taswira chanya kwa taifa.



Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, akijadiliana jambo na Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, katika mkutano wa mwaka wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Jimbo la Chalinze kuhusu utekelezaji wa ilani ya chama hicho, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kushughulikia tatizo la umeme kwa kasi

**Na Mwandishi Wetu,** PWANI

SERIKALI imeahidi kushughulikia tatizo la umeme nchini kwa kasi ili tatizo hilo limalizike katika kipindi kifupi kuanzia sasa.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alitoa ahadi hiyo ya serikali katika Mkutano Mkuu Maalum wa Jimbo la Chalinze wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025)

Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani.

Alisema, katika kipindi cha miezi sita inayokuja ukosefu wa umeme nchini utaisha baada ya serikali kuweka mikakati madhubuti ya kumaliza tatizo hilo nchini. Pia, watendaji wanafanya kazi ili Watanzania wapate umeme wa kutosha.

Katika hatua nyingine, Dk. Biteko aliagiza TANESCO kupeleka umeme katika Shule ya Sekondari ya Moreto ili iunganishwe na umeme mapema na amechangia kompyuta 10 kwa matumizi ya TEHAMA kuwasaidia wanafunzi.

Kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Dk. Biteko alipongeza juhudi zinazofanywa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kijamii ikiwamo ujenzi wa madarasa, zahanati na miundombinu muhimu na pia kufanya vizuri katika makusanyo ya mwaka ambayo imekusanya Sh. bilioni 15.

Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete alisema, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anatoa msukumo mkubwa kwenye maendeleo ya nchi na fedha hizo zinaelekezwa katika miradi mbalimbali ili kukuza uchumi wa nchi.

Vilevile, Dk. Kikwete amempongeza Dk. Biteko kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati hapa na kumsisitiza awe msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya serikali na kufanya kazi kwa bidii.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema mkoa wake unaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa shule, madaraja, vituo vya afya ili ukue kiuchumi na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi wake.

Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alisema, katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze imefanikiwa kutekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/25.

"Wananchi wamewezeshwa kiuchumi, hali ya uzalishaji katika kilimo, uvuvi, umwagiliaji, viwanda na biashara imeongezeka, miundombinu ya shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali ya wilaya imekamilika kwa asilimia kubwa na kwenye baadhi ya vijiji na kata ujenzi unaendelea," alisema.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash alisema wameshuhudia mabadiliko makubwa kimaendeleo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Sunshine wakiangalia hali ya mabwawa yao ya tope sumu hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uwekezaji tata Chunya waiibua NEMC ikigundua 'madudu' mradi wa mgodi

- Wakazi watoa mazito wanavyodhurika kiafya
- Yadaiwa ulikuwa mbioni kuuzwa kinyemela

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** CHUNYA

KWA kifupi, kuna matatizo kwenye mradi wa uzalishaji dhahabu katika Kata ya Matundasi, wilayani Chunya, mkoani Mbeya.

Wakazi wa kata hiyo wapatao 9,477 (Sensa ya mwaka 2012) wako hatarini kukumbwa na maradhi ya saratani na kujifungua watoto wenye ulemavu kutokana na utiririshaji kemikali toka migodini kwenda katika vyanzo vya maji.

Mwekezaji, kampuni inayoitwa Sunshine Mining (T) Limited imebainika kukiuka sheria na taratibu za uhifadhi mazingira, zikiendana na utendaji unaoacha maswali kwa mamlaka za umma, baadhi hazina majibu.

Imebainika kampuni hiyo ya uchimbaji madini inatitirisha kemikali toka mabwawa yake ya kuhifadhi tope sumu kwenda Mto Lupa unaopeleka maji Ziwa Rukwa, hivyo kuwaweka hatarini kiafya wanyama na mimea inayotegemea maji hayo.

Kampuni inazalisha dhahabu katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1.84 wilayani Chunya. Leseni ya uchimbaji: ML 588/2018. Itafika ukomo Machi 10, 2028, kwa mujibu wa Tume ya Madini.

Vilevile, unaporejea jina la Chunya, limo katika anwani ya uzalishaji madini kitaifa na harakati za kiserikali kutanua wigo wa uwekezaji wake, hasa dhahabu, zinafanyika kisasa na kwa ngazi ya viwanda.

Kama ilivyo kwa uwekezaji mwingine kokote duniani, 'vigezo na masharti kuzingatiwa'. Kwa nafasi ya pekee mgodini, mazingira huangaliwa kwa tafsiri pana ili kuhitimisha uhalali wa uzalishaji huo wa madini.

Hicho ndicho kilichoibua migongano kuanzia ngazi ya minong'ono kwa wenyeji kijijini Matundasi B na mamlaka za wilaya kabla ya ngazi ya juu kitaifa kuingilia kati na kubaini kuna matatizo yasiyoendana na masharti ya kisheria katika mgodi huo.

Baadhi ya wakazi wa Matundasi B wanazinyooshea kidole kampuni jirani za madini kwa kuharibu mazingira, wenyeji na viumbe hai mahali huko vinadhurika kutokana na kemikali zinazotiririshwa toka migodini na kuingizwa katika vyanzo vya maji.

Hilo sasa linaibua ukali wa serikali inayoendelea kuchukua hatua kwa kuzingatia sheria na miongozo mingine iliyowekwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, hatua za kimazingira zinazochukuliwa, zinaendana na kudhibiti maslahi yote ya umma na hakubaliani na utiririshaji kemikali unaofanywa na wawekezaji wilayani Chunya.

**KINACHOJIRI CHUNYA**

Vilio vya aina tatu vimetawala: Ardhi imeharibiwa; kuna madai kwamba maji hasa ya mito inayotegemewa yana sumu; na viumbe hai kama mifugo, pia wakazi wanadhurika. Watuhumiwa wakuu wa madhila wanatajwa ni kampuni za uchimbaji madini.

Mariam Jafari, mkazi wa Kitongoji cha Matundasi B, Kata ya Matundasi jirani na mgodi huo, anasema ni shuhuda wa maji taka kutoka migodini kutiririka kuingia katika Mto Lupa wanaotumia maji yake.

Huku akifafanua kwa lugha ya kiufundi, Mariam anadai maji hayo yana kemikali, akizitaja kwamba haziozi, zinatiririka katika mfumo wa maji mtoni, hata hatari ya athari kuhamia moja kwa moja kwa watumiaji wa maji ya mto kwa kunywa na huduma zinginezo.

"Hizo kemikali huwa haiishi na wala haijawahi kuoza. Zinakuwapo chini. Kwahiyo, utakapochota maji utafanyaje? Utazinywa!

"Kwa hiyo, hata mimi ukinipima, hata ukichukua nywele zangu, lazima utanikuta kemikali hizo ninazo. Kwanini? Yale maji yanazo, halafu zile sumu wanazochenjulia (cyanide au zebaki), yale marudio (mchanga wenye madini) ni sumu ambayo ni kali.

"Hata mnyama akinywa, hawezi kufika pale barabarani, hatua chache anakufa! Sisi kiafya, tupo hatarini asimilia mia. Nimeongea mara ya kwanza kwamba tunapata sumu, ambazo ni zile kemikali..." anatamka Mariam akiwasilisha hisia na malalamiko ya wakazi wenzake.

Hoja ya Mariam inaungwa mkono na Mzee Ambakisye John (65) kutoka kitongoji hicho, akiendeleza simulizi namna mifugo yao kama ng'ombe inavyokufa mtoni, hali kadhalika samaki na vyura wanaoishi katika maji hayo.

Kwa mujibu wa Mzee Ambakisye, hata majani wanayolisha mifugo yao, wanashuhudia athari za kiafya zinazodhuru viumbe hivyo, akirejea kwa binadamu, sehemu kubwa wanaookota samaki hao na kuwala huugua tumbo.

Mzee Ambakisye anaeleza hatua wanazochukua wakazi kujihami, akisema: "Wananchi hawajui wapi watakwenda kulalamika, watakwenda ofisi gani huko bomani (kwa Mkuu wa Wilaya), wataingia ofisi gani na Ofisa Mazingira hawaijui ofisi yake iko wapi, wa wilaya (Mkuu wa Wilaya) hawajui.

"Wangekuwa wanaweza kufika wakalalamika, walau ofisa kutembelea kwenye vijiji aangalie na aongee na wananchi wanapata madhara gani kufuatana na uchenjuaji wa madini.

"Madhara yamejitokeza mara nyingi, ng'ombe wamekufa, watu wenyewe wamekula samaki waliokufa kwa sababu ya sumu, wameugua matumbo na bado wanaendelea.

"Hatujui kama sumu zingine zinakula polepole baada ya miaka 20... ngapi huko, watu wengi watadhurika kwa sababu, maji tunayotumia ni kuanzia Mto Lupa wenyewe, Mto Mtundasi na Mto Jua Kali. Mvua ikinyesha, sumu hizo zinakwenda katika vyanzo vya maji. Mto Lupa tunatumia maji yake kufua, kunywa, kupikia!"

Mkazi mwingine wa eneo hilo, John Mwalukaga, anayejitambulisha kwa vitendo yu mweledi katika uchimbaji mdogo wa madini, anafafanua kwamba wao wakazi wanapotumia maji ya mazingira yao, huwashwa mwilini.

Hapo Mwalukaga ana ufafanuzi zaidi: "Mikono inababuka, kunawasha kwenye miguu, mikono, usoni. Kwahiyo, unakuta yawezekana baadaye kukawa na madhara makubwa zaidi.

"Na hata vyakula tunavyokula ni hatari kwa sababu ng'ombe wanakunywa hayo maji na sisi tunakula nyama yao na hatujui baadaye kutatokea nini."

Mwalukaga pia anaeleza namna uchenjuaji madini unavyotumia kemikali zenye sumu kali ambazo kwa sasa anadai zimetawala katika vyanzo muhimu vya maji Chunya.

Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Hussein Magala, anadai kutokuwa na taarifa za kutosha ingawa ana dokezo la utafiti rasmi wa kiserikali ambao umebaini kuwapo sumu katika vyanzo vyao vya maji.

**OFISA MAZINGIRA**

Yohana Ngurukila, Ofisa Mazingira Wilaya ya Chunya, anasema walibaini athari za kimazingira katika mradi wa Kampuni ya Sunshine Mining (T) Limited na kutoa taarifa NEMC ambao sasa wanachukua hatua dhidi ya kampuni hiyo.

Ngurukila anathibitisha kampuni hiyo inacho cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) na ilitimiza masharti ya kimazingira kabla ya kupewa kibali cha kuanza shughuli zake, lakini baadaye walibaini maji yaliyotiririka kutoka mgodini huko kwenda kwenye mazingira jirani.

"Tuliamua kuwaandikia barua NEMC baada ya kuona mgodi umesitisha shughuli toka mwaka 2021, lakini pale pana tope sumu, ni lazima zifanyike jitihada za makusudi. Ndiyo maana maofisa wa NEMC walifika kukagua.

"NEMC wamefanya jitihada nyingi ikiwa ni pamoja na kuchukua sampuli kwenda kuziangalia kiwango cha sumu kilichomo," anasema Ngurukila na kusisitiza taarifa zaidi kuhusu suala hilo ziko kwa NEMC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na NEMC ngazi ya taifa.

Ofisa huyo anawataka wachimbaji madini kutimiza matakwa ya sheria, kanuni na taratibu, akisisitiza si dhamira ya serikali kusuguana na wawekezaji.

**NEMC WANG'AKA**

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Gwamaka, amemwambia mwandishi kuwa wamebaini kampuni ya Sunshine Mining (T) Limited ilisitisha shughuli zake mwaka juzi na wamiliki wake, wako mbioni kuuza mradi huo kwa mwekezaji mwingine ambaye anasita kumtaja.

"Mtu mwingine anaweza akanunua mgodi pasipo kujua kuna mambo gani ambayo ni hatarishi, akawa ameyabeba pasipo mwenyewe kujua. Kwahiyo, tukaingilia kati.

"Sehemu kubwa ya watu ambao walikuwa wanataka kununua huo mtambo ni Watanzania... wangejikuta wanaingia kwenye gharama kubwa za kurejesha mazingira kwenye hali inayopaswa kufanyika.

"Wakajikuta baadaye katika matatizo makubwa na wale wengine (raia wa kigeni) wakawa wamekwishaondoka. Kwahiyo, lengo lilikuwa kwanza kusimamisha uuzaji wowote," anafafanua.

Dk. Gwamaka anaeleza azma ya NEMC kuwaita Sunshine ni kuwahoji sababu za kukiuka mkataba wa mazingira wenye tafsiri yake katika cheti walichopatiwa, ikiwamo kurejesha ubora wa ardhi katika hali yake ya asili.

Huku akidai walikuwa ka-

Inaendelea Ukurasa 16

## Bilioni 625/- kutumika kujenga kiwanda cha meli, meli mbili

**Na Restuta James**

SERIKALI inakusudia kutumia Sh. bilioni 626 kujenga kiwanda cha meli na meli mbili za mizigo zitakazofanya kazi katika Ziwa Victoria na Tanganyika.

Kampuni iliyoshinda kandarasi ya kutekeleza miradi hiyo mitatu ni Dearsan Shipyard ya Uturuki, ambayo imetia saini mkataba na Shirika la Huduma za Meli Tanzania (MSCL) jana katika hafla iliyoshuhudiwa na Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa katika Bandari ya Kigoma Ujiji.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Uchukuzi kwa vyombo vya habari jana, ilimnukuu Waziri Mbarawa akieleza kuwa ujenzi wa kiwanda hicho utachukua miaka miwili na meli zitajengwa ndani ya miaka mitatu.

Alisema kiwanda hicho kitakuwa kikubwa na cha kipekee kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Ujenzi wa kiwanda hiki utasaidia ujenzi wa meli kutoka nchi mbalimbali zinazotuzunguka kama vile Burundi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na nchi zingine mbalimbali kwa kuwa kiwanda kitakachojengwa ni kikubwa," alisema Prof. Mbarawa.

Waziri huyo alisema lengo la miradi hiyo ni kurahisisha na kuchochea biashara baina ya Tanzania na nchi jirani na kwamba nia ni kupunguza siku za kusafirisha mizigo ya nchi jirani ikiwamo ya Kongo inayotoka Dar es Salaam kutoka siku tano hadi saba za sasa hadi saa 24.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL, Erick Hamis, alisema ujenzi wa kiwanda cha meli unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 322.7 na kitakuwa na miundombinu ya kudumu ikiwamo chelezo yenye uwezo wa kupandisha na kushusha meli yenye uzito wa tani 5,000.

"Kiwanda hiki kitakuwa cha kwanza cha aina yake katika ukanda mzima wa maziwa makuu, kinatarajiwa kuwa na teknolojia ya kisasa katika ujenzi wa meli ikiwa ni pamoja na vifaa vya kisasa vya kukatia vyuma," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ujenzi wa meli ya mizigo katika Ziwa Tanganyika utagharimu Sh. bilioni 158.2 na itabeba tani 3,500 yakiwamo malori 25.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ujenzi wa meli ya mizigo katika Ziwa Victoria utagharimu Sh. bilioni 145 na itakuwa na uwezo wa kubeba tani 3,000 za mizigo yakiwamo malori na mabehewa.

SIKU YA MTOTO WA KIKE

# Waliokatisha masomo kwa ujauzito wafikiriwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewaita wadau kufanya utafiti kuhusu kurudisha shuleni watoto wa kike waliokatisha masomo kwasababu mbalimbali ikiwamo ujauzito ili kuona mafanikio na vikwazo walivyokabiliana navyo na kuja na mapendekezo yanayolenga kutekeleza azma ya kutomwacha mtoto yeyote nyuma kwenye elimu.

Katika utekelezaji wa Waraka wa Elimu namba tatu mwaka 2021 wa kuwarejesha shuleni wasichana waliokatiza masomo hadi sasa 7,995 wamerejea na wanaendelea na masomo kupitia mfumo rasmi na usio rasmi wa elimu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike. "Tunapenda kufanya tathmini ya zoezi lile hasa la kuwarudisha shuleni watoto wa kike walioacha masomo kwasababu ya ujauzito, kuona mafanikio na changamoto walizonazo ili kuangalia namna bora zaidi ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan."

"Nina salamu zangu kwa UNICEF (Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto) na naialika ishirikiane na wizara yetu kutoa rasilimali fedha katika kufanya utafiti kwa kufuatilia wote ambao wamerudi shule mmoja mmoja kumhoji kuangalia mazingira, mafanikio, changamoto na mapendekezo ya namna bora zaidi ya kutekeleza maelekezo haya ya Rais Samia ya kuhakikisha hakuna mtoto atakayeachwa nyuma kwenye elimu," alisema.

Alibainisha kuwa wanaoacha shule wengi zaidi ni watoto wa kiume, lakini angependa utafiti huo uanze kwa awamu ya kwanza kufuatilia mabinti waliorudi shuleni.

Aidha, alisema mafanikio mengine ambayo Tanzania inajivunia ni pamoja na mwaka 2022/23 wanafunzi 636 waliofaulu vizuri kwenye masomo ya sayansi ikiwamo wa kike 261 ambao ni sawa na asilimia 41 ya wanafunzi wamenufaika na Samia Scholarship.

Waziri Mkenda pia alisema idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu imeongezeka kwa asilimia 31 kutoka wanafunzi 423,025 na kati yao wa kike ni 177,905 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 555,166 kati yao wa kike ni 249,009 kwa mwaka 2022/23.

Kuhusu walionufaika na mikopo ya elimu ya juu, alisema idadi yao imeongezeka kutoka wanafunzi 131,659 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia 202,016 kwa mwaka 2022/23 na ongezeko hilo ni sawa na asilimia 53, miongoni mwa wanufaika ni wa kike 50,145 kwa mwaka 2019/20 na 85,793 kwa mwaka 2022/23 sawa na asilimia 71.

"Wizara imejenga shule mpya 26 za wasichana ambapo kila mkoa kwa Tanzania bara ni shule moja na shule nyingine moja kwa kila kata kwa watoto wa kike na wa kiume ili kupunguza umbali kutoka nyumbani kwenda shuleni jambo ambalo limepunguza changamoto ambazo wangekutana nazo wakati wa kwenda shule," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Husna Sekiboko, alisema Bunge na kamati haitakuwa kikwazo katika mipango ya serikali ya kumwendeleza na kumlinda mtoto wa kike nchini.

Mwakilishi wa UNICEF nchini, Dk. Daniel Baheta, alisema shirika hilo litaendelea kujitolea kuunga mkono jitihada za serikali kuwaendeleza wasichana na kuwawezesha huku akipongeza uamuzi wa kuruhusu wasichana waliopata ujauzito kurudi shule.

Mmoja wa wanufaika wa Mradi wa SEQUIP, Neema Chaopa, alimshukuru Rais Samia kwa kuwafuta machozi watoto wa kike kupitia mradi huo ambao wengi wao walikuwa wamekata tamaa baada ya kukatisha masomo yao kwa sababu mbalimbali.

"Kupitia mradi wa SEQUIP tumefutwa machozi tumerejesha ndoto zetu upya, tunasoma kupitia Taasisi ya Watu Wazima kuna mabinti walikuwa wanauza mboga huku wanasoma walipata ujauzito....," alisema.




Mkaguzi Msaidizi wa Polisi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kinondoni, Makala Khida, akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike yaliyoandaliwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), eneo la Mwananyamala, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kizimbani mashtaka kubaka, kumpa ujauzito mwanawe

**Na Halima Ikunji,** TABORA

HAMIS Said (37), mkazi wa Mtaa wa Nkokoto, Kata ya Igunga Mjini, amepandishwa kizimbani kwa tuhuma za kumpa ujauzito mtoto wake mwenye umri wa miaka 16 (jina limehifadhiwa) anayesoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Igunga Mjini.

Said alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Igunga na kusomewa mashtaka mawili.

Akisoma mashtaka hayo, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mashtaka Wilaya ya Igunga, Albanus Ndunguru, alidai mbele ya Hakimu Edda Kahindi kuwa mshtakiwa huyo anashtakiwa kwa tuhuma za makosa mawili.

Nduguru alidai katika shtaka la kwanza linalomkabili mshtakiwa Said kuwa ni kufanya mapenzi na mwanawe kinyume cha kifungu 158(1) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16, mapitio ya mwaka 2022.

Alidai kuwa kati ya mwaka 2018 na Juni 2023, mshtakiwa alitenda kosa la kufanya mapenzi na mwanawe.

Katika shtaka la pili linalomkabili mshtakiwa Said, Nduguru alidai kuwa mshtakiwa alimpa ujauzito mwanafunzi anayesoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Igunga Mjini mwenye umri wa miaka 16.

Alidai kuwa Juni mwaka huu, mshtakiwa alimpa ujauzito mwanafunzi. Ni kosa kwa kuzingatia kifungu cha 60 A kidogo cha tatu cha Sheria ya Elimu, Sura 353 ya mwaka 2019 inayozuia kutenda kosa hilo.

Mwendesha mashtaka alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, hivyo akaomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa hoja za awali.

Baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka hayo mawili, alikana kutenda makosa hayo. Kesi iliahirishwa hadi Oktoba 20 mwaka huu, huku mshtakiwa huyo akirejeshwa mahabusu baada ya kukosa dhamana.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# EWURA kazi iendelee wanaohujumu mafuta

**BAADHI** ya wafanyabiashara wa usafirishaji wa mafuta ya petroli na dizeli, wameamua kutumia mbinu ya kuhujumu sekta hiyo na kuwaumiza wananchi hasa wa hali ya chini kwa kuchelewesha kufikisha mafuta kwenye vituo husika wakisubiri kupanda kwa bei.

Mbinu hiyo pia imekuwa ikitumika kwenye baadhi ya vituo vya kujazia mafuta hayo na kusubiri mwisho wa mwezi wakati Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inapotangaza bei mpya ili wapate faida zaidi ya bei waliyonunulia.

Kitendo hiki kimekuwa kikisababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa nishati hiyo kwa kuongezewa gharama na pia kutoyapata mafuta wanapoyahitaji kwenye vituo kutokana na kufichwa.

Kutokana na tabia hiyo, EWURA imeamua kuvifungia vituo viwili vya mafuta, baada ya kubainika kuhodhi bidhaa ya nishati hiyo, huku baadhi vikificha kwenye malori na wengine kutumia mbinu ya kuyasafirisha kwa zaidi ya tano, maeneo yaliyo na umbali mfupi.

Vituo vilivyofungiwa ni kutoka Wilaya ya Chemba, vyote vya mkoani Dodoma ambavyo havitajihusisha na biashara hiyo kwa kipindi cha miezi sita huku mamlaka hiyo ikionya kuwa vitendo hivyo ni miongoni mwa vinavyochangia bei ya bidhaa hiyo kupanda.

Kwa kipindi cha miezi tisa, bei ya nishati hiyo imepanda kwa takribani shilingi 400 hadi 600, huku Januari 4, mwaka huu, EWURA ikitangaza bei ya petroli kwa mwezi huo, kuuzwa kwa rejareja kwa Sh. 2,819 na dizeli Sh. 3,295 na hadi kufikia Oktoba 4, mwaka huu, bei ya petroli kwa mkoa huo ikifikia Sh. 3,281 na dizeli Sh. 3,448 kwa lita moja.

Mamlaka hiyo mpaka sasa imeshavifungia vituo tisa mpaka sasa kutokana na kadhia hiyo.

Septemba 29, mwaka huu, EWURA ilivifungia vituo saba kwa miezi sita kwa makosa ya kuhodhi mafuta kinyume na sheria na imetangaza kuendelea na uchunguzi wa vituo vingine zaidi.

Kuanzia Julai, mwaka huu, kumekuwapo na matukio kwa baadhi maeneo hasa pembezoni mwa nchi kukosa mafuta hasa kipindi bei zinapoelekea kubadilishwa na kusababisha kuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi na madhara ya kiuchumi.

Pamoja na mafuta kuwapo nchini, changamoto ya upungufu katika maeneo mbalimbali, inachangiwa na baadhi ya wamiliki wa vituo vya kuuzia mafuta kwa makusudi kuamua kuhodhi, kujipatia maslahi haramu ya kibiashara.

EWURA imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisheria, ikiwamo kuvifungia baadhi ya vituo vilivyothibitika kuficha mafuta kinyume na kanuni na miongozo inayosimamia biashara ya mafuta nchini.

Septemba 16, mwaka huu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alipotembelea ofisi za EWURA, Dar es Salaam, aliwaonya baadhi ya watumishi ambao wanajihusisha na vitendo vya kuvujisha siri za mamlaka hiyo, siku chache kabla ya kutangazwa bei mpya kila mwezi.

Pia aliiagiza Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Mkurugenzi Mkuu EWURA, kupitia upya kasoro zilipo, zinazosababishwa na kutokana na watumishi hao na kujiridhisha, iwapo wapo wasio waaminifu wabainishwe na kufundishwa namna ya kuwa waaminifu.

Imebainika kuwapo watu wachache ndani ya EWURA, ambao si waaminifu wanaojihusisha na vitendo vya kuihujumu mamlaka kwa sababu siku ya ukaguzi wote wanakuwa na dharura, au kuna shida ya mafuta mamlaka inapokwenda kukagua wafanyabiashara wote wanakuwa wameshajua na kufunga vituo.

Imebainika kuwa sababu za upungufu wa mafuta baadhi ya mikoa, pamoja na kuwa na mafuta, ni wafanyabiashara kuchukua mafuta na kuchelewesha kuyafikisha vituoni, huku wengine wakiwa na mafuta kwenye visima, lakini hawauzi na kusababisha kuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vita afya ya akili mitaani, inavyojikita kukinga kuliko kuanza tiba

Na Beatrice Moses

**"AFYA** ya akili ni haki ya binadamu kwa wote." Ndiyo kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili, inayoadhimishwa kila Oktoba 10 ya kila mwaka. Ina mana ilifanyika juzi. Hapo kimsingi, imebeba maana kubwa inayoangaza ustawi wa jamii kwa ujumla.

Ni wazi kuwa afya ya akili ni mtaji mzuri kwa kila binadamu, inapotokea kuwa duni inakuwa ni changamoto ya aina yake ambayo pia kwa namna nyingine husababisha madhara makubwa ikiwamo ukatili, kutengwa ama kujitenga.

Shirika la Afya Duniani, WHO linatoa wito kwa serikali za kitaifa na za mitaa kuweka kipaumbele katika kupunguza mambo yanayojulikana kuwa hatari kwa afya ya akili ya watu.

Baadhi ya mambo yanayotajwa ni pamoja na ukata unaosababisha ugumu wa maisha, migogoro ya kijamii, ikiwamo ya wanandoa, hata vyombo kadhaa vya habari vinaripoti kushika kasi na kusababisha madhara ikiwamo mauaji.

kwa mujibu wa Ripoti ya Afya ya Akili iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) Mwaka 2017, kuwa ni mabadiliko ya kila mara kijamii, kutengwa na kijamii.

Vilevile, inatajwa mtindo wa maisha usiozingatia kanuni za kiafya, uhatarishi wa vitendo vya ukatili na ukiukwaji haki za binadamu.

Kuna sababu nyingi zimeorodheshwa, kama mikopo nayo inaweza kuwa sababu ya watu kuugua afya ya akili 'mkopo unapopewa jina la "kausha damu" kwa namna fulani inaweza kuchukuliwa kama mzaha, lakini ukweli wake kuna wanaoumia na mikopo kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kukosa elimu ya namna nzuri ya kutumia mikopo yao na kujipatia faida badala ya hasara.

Hutokea matukio, mtu anakopa na kisha anapoipata, anaitumia kwa mahitaji yake ya nyumbani, starehe na mengineyo na kisha anajiweka katika matarajio kuwa atamudu kuurejesha huo mkopo.

Serikali imewahi kufanya kampeni kadhaa ikiwamo ya malaria na imeonyesha mafanikio ya watu kuona umuhimu wa kulala ndani ya vyandarua, basi ni vyema pia kukaanzishwa kampeni za kupunguza mambo yanayosababisha matatizo kwa afya ya akili.

Kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwamo viongozi wa dini zote ni wadau kusaka ufumbuzi wa tatizo hili ambalo ni tishio kwa ustawi wa jamii kwa ujumla.

Kuna maoni ya umma sasa yanatawala, kwamba serikali ione umuhimu wa kuchukua hatua, ikiwamo kuwatumia vyema wasomi wa masuala ya ustawi wa jamii na saikolojia, ikiwezekana kila kwenye serikali ya mtaa, ili wasaidie kutoa ushauri muhimu.

Ni mtazamo kwamba inaweza kuleta matokeo mazuri ikiwamo kupunguza idadi ya wenye matatizo ya afya ya akili.

Mara kadhaa kumeshuhudiwa matangazo kwenye magazeti au madalali wa baadhi ya benki au taasisi za mikopo wakitangaza kuuza mali mbalimbali, ikiwamo nyumba za wadaiwa.

Hapo kama familia ndiyo, ni wazi kuwa wahusika wa kaya hiyo na hasa mkuu wake, anangukiwa na msongo wa mawazo.

Dalili za magonjwa ya akili zinazotajwa na wataalamu ni pamoja na kupoteza uwezo wa kufikiri vyema, kuwa na hofu zaidi, kuwa na msongo wa mawazo unaoathiri hadi mwonekano wa mwili.

Tatizo la afya ya akili linatajwa kuwa kichocheo kimojawapo kwa watu hasa wenye msongo au mfadhaiko kunywa pombe au kutumia vilevi vinginevyo wakijaribu kukabiliana yanayowasibu.

Mnamo Oktoba 10, mwaka jana, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu katika Kongamano la Kwanza la Kitaifa la Afya ya Akili, lililofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, akawataka wataalamu wa afya kujadili gharama za huduma za afya ya akili kuingizwa kwenye mfumo wa Bima ya afya.

Pia akawataka kujadili namna bora ya kuboresha huduma na kutoa maoni ya nini kifanyike ili kukabiliana na changamoto za Afya ya Akili na kuboresha Huduma za Saikolojia na Afya ya akili ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora.

Tujiulize, je mrejesho wa hayo maagizo upo wapi? maana kutibu saikolojia ni gharama ambazo zinapaswa kuingizwa kwenye bima

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Wizara ya Afya mwaka jana, Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa takriban milioni saba wenye magonjwa mbalimbali ya akili na matumizi ya dawa za kulevya.

Hao ni miongoni mwao zaidi ya watu milioni1.5 wanaoishi na ugonjwa wa sonona (Depression).

Hivi Karibuni, Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Baraka Makona, akabainisha kuwa changamoto ya matatizo ya kisaikolojia na afya ya akili, suluhu yake siyo hospitali pekee.

Akarejea kutanua wigo wa kutambua matatizo mengineyo yanayoigusa jamii na kuwa chanzo tatizo hilo, namna ya utatuzi sahihi, ikiwamo kuwahusisha viongozi wa dini katika utatuzi wa changamoto hizo.

HABARI KITAIFA

## Mahakama: Majangili kesi za wanyamapori wapewe adhabu kali

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imewaagiza waendesha mashtaka na mahakimu kutoa adhabu kali kwa majangili wanaopatikana na kesi za wazi za kutoweka kwa wanyamapori.

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapha Sayani, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya uendeshaji mashauri ya makosa ya wanyamapori na maliasili kwenye risala iliyosomwa kwa niaba yake na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro, Latifa Mansoor, Iliyoandaliwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

Jaji Sayani alisema, hafiriii wapo watakaopindisha kesi hizo zenye kuhatarisha kupotea kwa wanyamapori zikiwa na uwazi kwa ajili ya pesa kidogo.

Alisema ingawa majangili wataonekana wana uwezo wa kifedha kutokana na kuuza rasilimali za nchi na wahusika wa kesi wakibainika kuhusika kupokea rushwa na kupindisha kesi hizo.

Jaji Sayani alisema wanyapori 3,000 wapo katika hatari ya kutoweka kati ya wanyamaori milioni 10 waliopo nchini na kwamba mahakama inawashughulikia majangili wakiwamo wa meno ya tembo na nyara za serikali ambao hufikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 na kulipa fidia kwa serikali.

Alisema hata katika mafunzo hayo wameingiza mada ya rushwa ili kuwapa uelewa wa kutosha na kuwafanya kuboresha taaluma zao na hivyo kuwa wasimamizi wazuri wa mashauri hayo hasa yanapojitokeza.

Alisema majangili wanapojitajirisha kupitia wanyamapori na misitu kiharamu wasiposhughulikiwa faida wanazozipata zinatumika katika vitu vingi vya haramu ikiwamo kufanya ugaidi na kuwezesha vitu vingi haramu duniani.

Kadhalika, alisema mahakama imeamua kutoa mafunzo hayo ili kuwafanya majaji na mahakimu kuondokana na makosa ya kiufundi yanayosababisha majangili kuachiwa hata pale watakapokuwa wamefanya makosa kwa kutoa adhabu isiyostahili.

"Kuna baadhi ya kesi ambazo hazijapelelezwa vizuri, hivyo unakuta jangili anatoka kwa ajili tu kuna makosa ya kiufundi katika upelelezi, sasa hilo ndio wanataka walitibu katika haya mafunzo," alisema Sayani.

Mkurugenzi wa mafunzo ya kimahakama kutoka Chuo cha Uongozi wa mahakama Lushoto (IJA), Patricia Kisinda, alisema wanatarajia kutoa mafunzo hayo kwa maofisa wa mahakama zaidi ya 757 kutoka mikoa mbalimbali nchini na wameanza na mikoa mitano ikiwamo ya Morogoro, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Pwani.

Kisinda alisema wameamua kugusa wanyamapori na maliasili kwasababu ni eneo nyeti katika uchumi wa nchi na kuna changamoto nyingi katika uendeshaji wa mashauri ya wanyamapori mahakamani na baada ya tathmini ya mafunzo yaliyopita wameona kuna tija.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la PAMS Foundation, Samson Kasala, alisema katika kushirikiana na serikali na wananchi kuhamasisha kuelewa umuhimu wa maliasili wanafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha majangili, waporaji, wanaohusika kutenda makosa ya jinai wanashughulikiwa na mkono wa sheria.

Mafunzo hayo yamewashirikisha majaji wa mahakama kuu, mahakimu, waendesha mashataka na wapelelezi.



Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Morogoro, Neema Haule, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya sheria na kanuni za ulinzi kwa watoa taarifa na mashahidi kwa waandishi wa habari mjini Morogoro juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Silaa kushughulikia watumishi Wizara Ardhi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amesema kuanzia sasa mtumishi yeyote wa wizara hiyo atakaye kiuka miiko na maadili ya kazi hatavumiliwa.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi na watumishi wa sekta ya ardhi Mkoa wa Singida akiwa kwenye ziara yake ya kikazi ya siku moja ya kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Alisema, kuna migogoro ya ardhi ambayo inatatulika na mingi inasababishwa na utendaji mbovu wa baadhi ya waliopewa kusimamia kazi hiyo na wanapofanya makosa wanahamishwa kutoka sehemu alipofanyia kosa na kupelekwa kituo kingine cha kazi jambo ambalo katika kipindi chake hataliendekeza.

"Mfanyakazi atakayefanya kosa nitamalizana naye papo hapo sitahitaji kumpeleka kwingine," alisema Silaa. ingawa hakufafanua atamalizana naye kivipi mfanyakazi huyo atakayebainika kutenda kosa.

Aliwataka wafanyakazi wa wizara hiyo kufanya kazi zao kwa kufuata sheria na haki akiamini kuwa ni wanataaluma.

Aidha, aliwaelekeza watendaji wa sekta ya ardhi nchini ndani ya siku 100 kuanzia Septemba 4, 2023 kutatua migogoro ya ardhi ili kuwafanya wananchi kuwa na imani na serikali yao na kuifurahia wizara hiyo.

Alisema hatapenda kuona wananchi wakiinua mabango pale viongozi wa kitaifa wanapokuwa kwenye ziara katika maeneo mbalimbali wakilalamikia migogoro ya ardhi.

Alipongeza Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Singida kwa umahiri na ustadi wa utendaji katika zana pana ya kushughulikia migogoro mbalimbali ya ardhi sambamba na hatua nzuri za upimaji, umilikishaji na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi mkoani hapa.

Alilipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa ukusanyaji madhubuti wa mapato na ufanisi wa kiutendaji huku akiwataka watendaji kuendelea kuchapa kazi wakati serikali inaangalia namna ya kutatua changamoto zilizopo.

Naye Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Singida, Shamim Hoza alimhakikishia waziri kwamba wafanyakazi watazingatia maagizo yote yaliyotolewa kwa tija, ukuaji na mustakabari mzuri wa sekta nzima ya ardhi ndani ya mkoa huo.

Hoza alishauri kuwapo wa dhana ya ushirikishwaji baina ya watumishi wa sekta ya ardhi katika kutekeleza majukumu mbalimbali ili kuondoa migongano ambayo huathiri utendaji ndani ya sekta hiyo.

Akizungumzia mafanikio alisema ofisi yao kwa mwaka 2021 imefanikiwa kuandaa michoro 61 kwenye viwanja 19,620 na kueleza kuwa idadi hiyo inapanda kadri wanavyoendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuwa changamoto kubwa waliyonayo ni uhaba wa watumishi katika kada zote, kuwa na gari moja na ufinyu wa bajeti.

Naye Meneja wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Mkoa wa Singida, Judith Mwalongo alisema mkoa huo una jumla ya viwanja 105, vilivyoendelezwa ni 38 na visivyoendelezwa ni 67 na kuwa vipo katika maeneo tofauti.

Alisema Mkoa wa Singida una jumla ya majengo 39 yakiwa na jumla ya nyumba (units) 171, asilimia 90 ya nyumba hizo zipo katikati ya mji wa Singida.

Mwalongo alisisitiza kuwa shirika hilo limefanikiwa kukusanya mapato maradufu zaidi ya matarajio yaliyowekwa.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Walimu wakuu waliosimamishwa kupisha uchunguzi wasamehewa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewasamehe na kuwarejesha kwenye nafasi zao walimu wakuu watano wa shule za msingi wilayani Kyela waliosimamishwa kupisha uchunguzi wa matumizi ya fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule zao.

Homera pia ameagiza Ofisa Manunuzi wa Halmashauri hiyo, Milly Masare na mhandisi kuendelea kusimamishwa mpaka uchunguzi wa miradi hiyo utakapokamilika.

Walimu wakuu waliokuwa wamesimamishwa ni wa Shule za Msingi Kasumulu, Lubele, Mababu na Mapinduzi ambao walishindwa kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa wakati.

Homera aliwasimamisha watumishi hao Septemba 19 mwaka huu alipokuwa kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hasa inayohusu elimu.

Juzi Homera alitangaza kuwasamehe walimu hao baada ya kutembelea shule hizo na kubaini kuwa ujenzi wa vyumba hivyo umekamilika na kwa viwango vilivyokuwa vinatakiwa.

Alisema walimu hao walifanya makosa ambayo walilazimishwa na ofisa ununuzi na mhandisi wa halmashauri, jambo ambalo liliwafanya waonekane wakosaji.

"Hawa waliamua kufa na tai shingoni ndio maana yakawakuta haya yaliyowakuta. Sasa hili ni fundisho kwa walimu wengine kwamba ukiona umepewa mradi shuleni kwako, usimamie lakini kila kitu unalazimishwa kununua kwenye baadhi ya maduka, lazima ushtuke," alisema Homera.

Aliwataka walimu hao na wengine wote kuwa makini wanaposimamia miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye shule zao ili kuepuka kujiingiza kwenye matatizo ya kuwa watu wa kupitisha vitu ambavyo vinawarudia.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22, mbali na mambo mengine, imeangazia utekelezaji wa miradi ya ujenzi shuleni na vituo vya afya, mkaguzi huyo akikosoa walimu kutumiwa na serikali kusimamia miradi hiyo.



Mkurugenzi Mwenza wa Shule ya Msingi na Sekondari ya St. Rosalia ya Kinyerezi, Ilala jijini Dar es Salaam, Lilll Asela Edward (katikati), akizungumza wakati wa mahafali ya 10 ya darasa la saba shuleni hapo, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa shule hiyo, Paul Siaga na (kulia) ni Meneja wa CRDB Mbezi Mwisho, John Magwisha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yaanza kampeni kuondoa mita za zamani

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limetangaza kampeni ya kuondoa mita zote za zamani na kuwawekea mpya za kisasa wateja wake ikiwa ni sehemu ya kuboresha huduma.

Limesema kazi hiyo ya kubadilisha mita zinazoanzia na namba 04, 05 inatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi ujao na hakuna mwananchi ambaye atatozwa fedha kwa kubadilishiwa mita.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Meneja Mawasiliano wa shirika hilo, Irene Marobe, alipozungumza na Nipashe kuhusu maboresho yanayofanywa na shirika.

Irene alisema, shirika limeamua kubadili mita hizo kwa kuwa ni toleo la zamani na wanatarajia kuwa na mabadiliko ya kimfumo hivi karibuni, hivyo mita hizo hazitakuwa na sifa ya kupokea mabadiliko hayo.

Alisema, ndiyo sababu shirika limeanzisha kampeni ya kuwajulisha wateja wake wenye mita hizo watoe taarifa kwenye ofisi za shirika hilo au wapige namba za huduma kwa wateja ili wafiwe na kuziondoa.

Alisema shirika lina taarifa za wateja wake nchi nzima. Mita hizo zilikuwa toleo la mwanzo na la zamani wakati huduma ya Luku inaanza mwaka 1996, yaani miaka 27 iliyopita.

"Kipindi hicho wateja wetu walikuwa wanaunganishwa umeme kwa kutumia taarifa chache kama majina na namba ya sanduku la barua, taarifa ya namba za simu zilipatikana kwa wachache kutokana na uchache wa mitandao ya simu.

"Kwa kipindi hicho pamoja na hayo kumbukumbu zetu zilikuwa zikihifadhiwa kwenye kadi na kufanya kazi ya kuwafikia wateja wengi kuwa gumu," alisema.

Alisema kwa wateja ambao watakuwa hawajabadilishiwa mita zao mpaka kufikia mwisho wa kampeni hiyo ambayo ni Novemba 10 mwaka huu, mfumo utalazimika kuwafungia na wahusika watashindwa kununua umeme hadi watakapopiga simu TANESCO ambao watawafikia waliko na kuwapa huduma.

Irene pia alisema hatua ya kuwaunganishia wateja umeme kidijitali imeleta mafanikio makubwa kwa kuwa wateja wamekuwa wanaunganishwa umeme ndani ya siku tatu au nne wanapoomba umeme kwa njia hiyo.

Alisema mfumo huo unamwezesha mteja kuomba umeme na anapokamilisha mahitaji yaliyomo kwenye mfumo anafungiwa umeme bila kulazimika kwenda ofisi za TANESCO kama ilivyokuwa zamani.

Alisema kuanzishwa kwa kituo hicho cha miito ya simu ni sehemu ya mikakati ya shirika kurahisisha upatikanaji huduma ya umeme kwa kuwa mteja akipata changamoto inakuwa rahisi kuwasiliana na kumfikia kwa haraka.

Kuhusu miezi sita waliyopewa na Rais kuondoa changamoto ya umeme, Irene alisema mabadiliko makubwa ya kimfumo ambayo yanaendelea kwa sasa yanawapa uhakika kwamba watafikia malengo hayo waliyopewa.

Irene aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya umeme kwa kuwa uzoefu unaonyesha kwenye baadhi ya maeneo wananchi wamekuwa wanaihujumu na kulisababishia hasara kubwa.

Alisema wamekuwa wanapata ripoti za matukio mengi ya aina hiyo kwenye mikoa mbalimbali na wanaohusika wamekuwa wakichukuliwa hatua na alitoa rai kwa kila Mtanzania kuwa mlinzi wa miundombinu ya umeme.

"Sisi tunatarajia tunapoweka miundombinu ya umeme iwanufaishe wananchi wote. Sasa wanapoiharibu tunalazimika kununua upya wakati zile fedha zingetumika kuanzisha miradi mingine ya kuwaunganishia umeme maeneo ambayo hawana umeme," alisema

# Machifu kuanza 'Royal Tour' kwa wakuu wa nchi wastaafu

**Na Romana Mallya**

MACHIFU na vijana wameandaa utaratibu kinachoitwa 'Royal Tour', wakitembelea wakuu wa nchi kuanzia awamu ya kwanza hadi ya sasa ili kujifunza mambo mbalimbali likiwamo la maadili.

Jijini Dar es Salaam juzi, Chifu William Machimu kutoka Mwanza, akizungumza kwa niaba ya wenzake, aliwaambia waandishi wa habari kuwa kwa sasa nchi inahitaji kukaa pamoja kumuunga mkono Chifu Hangaya, Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tunapaswa kumuunga mkono Chifu Angaya hasa kuhusu habari za mmomonyoko wa maadili na namna ya Watanzania wanapaswa kuishi katika maadili, mila na tamaduni za Mtanzania," alisema.

Alisema Royal Tour imeandaliwa na Taasisi ya Wafikiriaji Duniani ambayo itawahusisha machifu na vijana kwenda kwa viongozi hao.

Chifu Machimu alitaja malengo mengine ya ziara hiyo ni kuwafundisha na kuwakumbusha vijana historia ya nchi kupitia viongozi ili kujua namna wanavyopaswa kuishi na kulinda mila na tamaduni za Kitanzania kama wao walivyofanya wakiwa vijana.

Alisema machifu na vijana watakwenda nyumbani kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Aman Abeid Karume, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Dk. Jakaya Kikwete na baadaye ziara itahitimishwa Zanzibar kwa Mama wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema hitimisho la ziara hiyo Zanzibar linatarajiwa kuwakutanisha wakuu wa nchi ambapo kutakuwa na michezo, ngoma na vyakula vya asili.

Alibainisha kuwa ziara hiyo inatokana na mawazo aliyotoa Rais Samia kwa taifa alipokutana na vijana mkoani Mwanza, akilitaka kundi hilo kujiandaa kwa kuwa nchi ni mali yao.

Pia alisema alipokutana na viongozi wa wanafunzi wa elimu ya juu Ikulu, aliwataka vijana wawalinde wadogo zao kitabia kwa kuwafundisha maadili.

Alisema katika utawala wake, Rais Samia amekuwa akihakikisha nafasi mbalimbali za uteuzi anazofanya, kundi la vijana haliachwi nyuma.

"Tumekutana leo (juzi) hapa machifu na baadhi ya vijana wa mkoa yote Tanzania kuzungumza malengo sahihi ya kuangalia ni namna gani mila na desturi za Mtanzania zinalindwa," alisema.

Kiongozi wa Kimila, Jadi asili na Utamaduni kutoka himaya ya Nyarutambwe Manyovu, Kigoma, Mfalme Dk. Fadhili alisema kwa sasa kuna baadhi ya watu hawafanyi kazi tena, wanaishia kwenye maombi au kwenda kwa waganga.

Dk. Fadhili ambaye ni Katibu Mkuu Muungano wa Falme za Afrika na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Wafikiriaji Duniani, alisema wapo wanaokwenda kwa waganga wakitaka utajiri, lakini wanapowauliza wanajishughulisha na nini wanasema hawana kazi.

"Sasa unajiuliza mtu hana kazi unakuja kwangu unataka utajiri. Msihangaike kuja kwetu kutaka utajiri, njooni tuwape ushauri kwa kuwa ndani ya jamii kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuwapa mafanikio.

"Kuna wengine hawajui hii nchi ni yao, wanajijua ni wananchi ila hawana uhakika kwa kuhisi kama nchi ni yao ili kutoa kipaumbele kusimamia rasilimali za nchi yao," alisema.

Katibu Mkuu wa Taifa wa Taasisi ya Wafikiriaji Duniani, Kasianus Nkwenge, alisema wamekutaka katika kikao cha kwanza cha ziara hiyo itakayohusisha marais wa pande zote.

Alisema kaulimbiu ya ziara hiyo inasema 'uzalendo kwanza, ninaipenda nchi yangu, rasilimali ni zetu, nchi ni yetu, serikali ni yetu na watu ndiyo sisi, tushikamane kwa pamoja kuijenga nchi yetu."



## Jenista: Vijana hawana ubunifu wa kuondoa tatizo la ajira

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uratibu, Sera na Bunge), Jenista Mhagama, amesema licha ya kanzidata ya sensa kuonyesha asilimia 55.6 ya vijana ndio nguvu kazi ya taifa, lakini kundi hilo bado halijapata ubunifu na ujuzi ili kuondoa tatizo la ajira linalowakabili hivi sasa.

Kutokana na hali hiyo ameelekeza vijana wasiachwe peke yao, bali wasaidiwe kupata ubunifu na ujuzi huo.

Mhagama, alimwakilisha jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Vijana Kitaifa, yanayoendelea katika Mji wa Babati, mkoani Manyara, kuelekea Oktoba 14 siku ya kilele cha uzimaji wa Mwenge wa Uhuru.

Alisema kwa kuwa vijana wana uwezo mkubwa kufanya mambo mbalimbali, hivyo ili kulinda ubunifu na ujuzi watakaopatiwa ni vyema wakapatiwa mitaji ili waendeleze ubunifu wao.

"Tungependa vijana mfanye ubunifu mpya na mataifa yaliyoendelea yalianza na viwanda vidogo vidogo na sisi tuwawekee mazingira mazuri waweze kufanya ubunifu,"alisema Mhagama.

Aidha, alizitaka benki kutoa mikopo nafuu yenye riba nafuu kwa vijana mpaka vijijini ili waweze kufanya mambo makubwa.

Alisema ni vizuri mfuko wa vijana usaidie kuwaibua vijana kwa kuwa ndiyo nguvu kazi ambao wako mil. 21.3, nchi nzima, huku akisema asilimia 55.6 ndiyo nguvu kazi ya vijana wa Tanzania.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, alisema wataendelea kuwawezesha vijana mikopo inayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Mark Bryan, alisema katika kulisaidia kundi hilo kufikia ndoto zao, shirika hilo linaendesha programu za uzazi na haki ambazo zimewafikia vijana 125,000.

Aidha, alisema wanasaidia ujasiriamali, uongozi na ujuzi wa elimu wa kuwajengea uwezo ili waweze kujiamini vijana.

# Mangariba wasalimu amri kwa kamati ya kutokomeza ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MANGARIBA wawili mashuhuri mkoani Kilimanjaro, wanaosifika kwa kukeketa vichanga na wasichana, wamesalimu amri na kutangaza kuachana na kazi hiyo.

Kusalimu amri huko kumetokana na kubanwa na Kamati ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) katika Kijiji cha Mawala, Wilaya ya Moshi.

Waliokubali kwa maandishi, kuacha kukeketa watoto wachanga na wasichana wa jamii ya kifugaji ya kimasai katika ukanda wa tambarare wa Kahe, ni Ruth Merinyi na Anjelina Jackson.

Akizungumza jana katika kikao kazi cha kutoa mrejesho wa shughuli walizozifanya wajumbe wa MTAKUWWA katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja, Katibu wa Dawati la Kupinga Ukatili, Kata ya Kahe Magharibi, Jonas Mlay, alisema mangariba hao wamekiri kwa barua (Nipashe imeiona nakala yake), kuendesha ukeketaji kwa njia ya usiri, licha ya vitendo hivyo kuwa haramu kwa Watanzania.

Kwa mujibu wa barua hiyo, mangariba hao walitangaza kuachana rasmi na kazi hiyo Septemba 25, mwaka huu.

Kamati hiyo imepata mafanikio chanya, baada ya kupatiwa mafunzo maalum na Shirika lisilo la kiserikali la TUSONGE CDO, linalotekeleza Mradi wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, chini ya ufadhili wa The Foundation For Civil Society.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, hivi karibuni, alinukuliwa akisisitiza kuwa baadhi ya mangariba wanatishiwa, na hata kutengwa na jamii zao baada ya kuacha vitendo hivyo vya kikatili, akisisitiza kuwa serikali itawalinda na kuwatetea kwa nguvu zote bila kuchoka.

"Ukeketaji ni ukataji wa sehemu za siri za mwanamke. Ukataji huo unahusisha maeneo nyeti, na ni kitendo chochote kinachoharibu uke kutokana na sababu ambazo sio za kimatibabu.

"Kimsingi, ukeketaji unaumiza wanawake na wasichana kimaungo na kiakili, na hakuna faida yoyote ya kitabibu wakati wa kitendo hicho. Zaidi ya kuchangia huzuni, na kuharibu uhusiano wa wanawake na vile wanavyojihisi."

Ofisa Mradi wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kutoka Shirika la TUSONGE CDO, Eva Minja, alisema kamati hiyo ya MTAKUWWA, baada ya kujengewa uwezo imepewa jukumu la kufuatilia na kupambana na vitendo hivyo katika Kata ya Kahe Magharibi.

"Mradi huu unaotekelezwa katika Kata ya Kahe Magharibi, walengwa wetu ni wanawake pamoja na watoto, kwa sababu lengo la mradi ni kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

"Mpaka sasa tumeweza kuwafikia wanufaika wetu wa moja kwa moja wanawake 150, watoto ambao ni wanafunzi 90, ambao tumewaweka katika mfumo wa klabu na tumewaelimisha kuhusu masuala yanayohusu watoto kujua haki zao.

Lakini kujua wajibu wao kama watoto, kuongelea maeneo ambayo ni hatarishi na yasiyo hatarishi na wapi wanaweza kwenda kutoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya ukatili."



Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Manyara, Mhandisi Walter Kirita (katikati), akizungumza na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Peter Toima (kulia) na Meneja wa RUWASA Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Joanes Martine (wa pili kulia), baada ya Mwenge wa Uhuru kuzindua mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 292.8 katika Kijiji cha Emboreet juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi watishia kuandamana kudai fidia kwa JWTZ

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MGOGORO mpya unanukia katika Kata za Moshono na Mlangarini, mkoani Arusha, baada ya wakazi wa maeneo hayo kutishia kuandamana ili kuishinikiza serikali kuingilia kati, sakata la malipo ya fidia ya ardhi yao iliyotwaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Wakati wananchi hao wakitishia kufanya hivyo, JWTZ kupitia Mkuu wa Kikosi cha 977, Kanali Hamis Kinguye, amewatoa hofu wananchi hao, akisisitiza kuwa malipo yao yapo, na yanashughulikiwa ngazi za juu.

Kwa nyakati tofauti jana na juzi, zaidi ya wakazi 500 wa maeneo hayo walieleza masikitiko yao kuhusu kuchelewa kwa malipo hayo ya fidia, kwa muda wa miezi 10 sasa.

Akizungumzia mpango wao huo, akiwa nje ya Ofisi ya Mtendaji Kata ya Moshono, Mosses Kivuyo, alisema Januari 30 mwaka huu, walifika katika eneo lao wataalamu wa ardhi kutoka Halmashauri ya Arusha na Halmashauri ya Jiji la Arusha, maofisa wa jeshi na wawakilishi wa wananchi, na kupima maeneo yao.

Alisema baada ya kuyapima, waliyafanyia tathmini na kila mwananchi, alijulishwa kiasi cha malipo ya ardhi yake.

"Baada ya kufanya tathmini wataalamu hao waliwajulisha wananchi kuwa malipo yao yangefanyika kati ya mwezi Mei na Juni mwaka huu lakini hadi leo Oktoba hakuna taarifa zozote juu ya malipo yetu na tunaishi kwa mateso makubwa"alisema Kivuyo. Mkazi mwingine wa Moshono, Emmanuel Masamaki, yeye aliiomba serikali kuwahudumia wananchi hao kwa kuwapatia chakula, wakati wanasubiri malipo yao ambayo hadi sasa, bado hayajajulikana watalipwa lini.

"Jeshi walitaka maeneo yetu kwa ajili ya shughuli zao, sisi hatukupinga, tulikubaliana nao wakapima maeneo yetu toka Januari mwaka huu na walituahidi ndani ya miezi miwili au mitatu, tutalipwa na wakatuzuia kulima.

"Lakini cha ajabu hadi leo, hawajatulipa chochote tunateseka na njaa na baadhi ya wenzetu wamekufa bila kufaidi malipo yao,"alisema Masamaki.

Kutokana na hali hiyo, Masamaki aliiomba serikali kuharakisha malipo yao ili kuwapa fursa wananchi hao kutafuta maeneo mengine ya kilimo ili kunusuru familia zao na njaa.

Mwananchi mwingine, Paulo Mollel, mkazi wa Kata ya Mlangarini, alisema hadi kufikia leo, hakuna malipo yoyote waliyopokea na wanazidi kuteseka.

Alipotafutwa kuzungumzia malalamiko hayo, Naibu Kamishna wa Ardhi, Mkoa wa Arusha, Jofrey Mwamsojo, alisema anayafahamu madai ya wananchi hao, huku akiahidi kushughulikia jambo hilo kwa kuwasiliana na mamlaka za jeshi na serikali.

Mwamsojo, aliahidi ndani ya siku 10 zijazo atakuwa amepata majibu ya uhakika kuhusu jambo hilo na atayapeleka kwa maandishi kwenye ofisi za kata hizo mbili.

Hata hivyo, Mkuu wa Kikosi cha 977, Kanali Hamis Kinguye, akifafanua kuhusu madai hayo alisema: "Hao wananchi waambie waondoe hofu, serikali haimrushi mtu. Malipo yao yanashughulikiwa na hakuna haja ya kuandamana na muda wowote watajulishwa."





# Mbaroni tuhuma kumtorosha binti akawe m'kazi wa ndani

**Na Said Sindo,** GEITA

MAMA mmoja Basiliana Suru mkazi wa Buhalahala Halmashauri ya Mji wa Geita amefikishwa katika ofisi za serikali ya mtaa akidaiwa kumrubuni na kumtorosha mwanafunzi aliyemaliza darasa la saba (jina limehifadhiwa) kwenda Arusha kufanya kazi za ndani, kwa makubaliano ya malipo ya Sh.75,000 bila wazazi wake kujua.

Taarifa za kupotea kwa binti huyo (16) zilianza kusambaa kutoka kwa watoto wenzake baada ya kutoonekana nyumbani wakidai walimwona akipanda bajaji na mama huyo.

Baba mlezi wa binti huyo, Kulwa Samike alieleza kuwa baada ya kutomwona nyumbani kwa muda mrefu walitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Mtaa, kuanzisha uchunguzi wa kubaini mtoto huyo alikoelekea.

"Baada ya kumtafuta kwa muda binti huyo alipiga simu ya mama yake mlezi akitaka kumjulia hali ndipo akaeleza kuwa amepelekwa Arusha kufanya kazi na analipwa Sh.75,000 na kumtaja mama huyu kuwa yeye ndiye aliyemsafirisha," alieleza Samike.

Dada wa mtoto huyo, Shelida Kulwa, alisema kuwa binti huyo siyo ndugu yao wa damu kwani aliokotwa akiwa na miaka nane, licha ya juhudi za kufuatilia kwa matangazo kupata ndugu zake ziligonga mwamba hivyo kuishi naye kama ndugu wa damu.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Jonathan Hery, alithibitisha kupokea mtuhumiwa huyo ambaye hata hivyo alikana kuhusika na tukio hilo.

Basiliana Suru, anayetuhumiwa kuhusika katika kumtorosha binti huyo alisema kuwa wakati binti huyo anaondoka walipanda bajaji moja na kutaja kigezo hicho ndicho kimetumika na binti huyo kumsingizia kuwa alimtorosha.




Mfanyabiashara Rachel Sanga kutoka Makambako mkoani Njombe, akipokea tiketi pamoja hati ya kusafiria kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali cha NBC, Mussa Mwinyidaho (kulia), jijini Dar es Salaam jana akiwa ni mmoja wa wafanyabiashara wanaokwenda nchini China, kushiriki maonyesho ya uagizaji na uuzaji wa bidhaa za nchi hiyo maarufu kama Canton Fair, yanayotarajiwa kufanyika hivi karibuni huko Guangzhou, safari iliyoratibiwa na NBC B-Club. Kulia ni Mratibu wa safari hiyo kutoka kampuni ya TBMC, Sarah Mauki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Agundua mfumo wa kudhibiti ajali za treni katika vivuko

**Na Benny Kingson,** TABORA

MWANAFUNZI kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Alvin Anton (28), amebuni mfumo wa ulinzi wa njia za reli utakaosaidia kupunguza na kudhibiti ajali zinazotokea katika vivuko vya reli nchini.

Mwanafunzi huyo aligundua mfumo huo akiwa na lengo la kuwezesha vyombo vingine vya usafiri na waendao kwa miguu kusimama pindi wanapoona taa zimewaka na geti limefunga njia ikiashiria kuna treni itapita kwenye eneo hilo la makutano.

Akielezea mfumo huo katika banda la chuo hicho, Alvin aliiomba serikali kupitia Wizara za Uchukuzi na Mambo ya Ndani kumuunga mkono na kumwezesha kufikia ndoto zake za kuweka mfumo huo katika vitendo.

Alisema mfumo huo utasaidia kuondoa kero ya alama zilizopo sasa katika vivuko vya njia ya reli ambazo zimepitwa na wakati na kwamba ana imani ata mfumo wa alama unatumiwa kuruhusu ama kutoruhusu treni kuingia katika vituo zimepitwa na wakati.

Naye Daniel Welema kutoka Wizara ya Uchukuzi alisema kuwa mfumo huo ni mzuri endapo serikali wakautumia kufunga kwenye reli ya kisasa na hata reli ya kawaida.

Aidha, alikitaka chuo hicho kutafuta vyanzo vya mapato ili kuendeleza mfumo huu na kuutangaza kitaifa na kimataifa ili kupata masoko na kulisaidia taifa kupiga hatua na kuendana na teknolojia.

Naye Ofisa Usafirishaji kutoka Wizara ya Uchukuzi, Bahati Benjamin, alisema kuwa mfumo huo utasaidia kuimarisha masuala ya usalama katika njia za reli na barabara.

Alisema kuwa NIT wanatakiwa kuhakikisha wanachangamkia fursa iliyoibuliwa na mwanafunzi wao na kuitumia kwa faida yao na kukiletea chuo sifa.

## Wawakumbusha wazazi kuwapa elimu watoto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BARAZA la Wazee Taifa limewakumbusha wazazi kuhakikisha wanawapa haki za kielimu watoto wao ili waweze kuwasaidia katika maisha yao ya uzeeni.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu wa baraza hilo, Anderson Lymo, wakati wa kuagwa mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Wilfred Bilago, aliyefariki dunia Oktoba saba mwaka huu akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani Bugando.

Alisema, wazazi na walezi wengi wanakosa mahitaji yao wanapozeeka na kuwa ombaomba mitaani kwa sababu ya kushindwa kuwalea watoto wao katika misingi ya kiimani na kuwasomesha.

Lymo alisema familia ambazo wazazi wamesomesha watoto wao vyema na kuwajenga katika maadili, watoto wanawakumbuka wazazi wao, kuwalea na kuwapatia mahitaji.

Alisema, Manispaa ya Kahama ina wazee 6,692 kati ya hao wazee 5,036 wameshapata bima, hivyo kuwahimiza vijana kuwakatia bima wazee wao kuwapa uhakika wa matibabu.

Naye Mzee Laurent Nkwabi alisema kushindwa kuwasomesha watoto kunasababisha watoto wa kike kupata mimba wakiwa nyumbani.

Mkazi wa Nyahanga, Samweli Paschal alisema: "Unaweza kuwasomesha watoto hadi wakapata kazi lakini wakashindwa kukusaidia kipindi cha uzeeni, hivyo ni vema kila siku wazazi wakapata muda angalau wa saa moja yakuzungumza na watoto wao na kuwasisitiza kupendana na kusaidiana siku zote".

**Alisema, wazazi na walezi wengi wanakosa mahitaji yao wanapozeeka na kuwa ombaomba mitaani kwa sababu ya kushindwa kuwalea watoto wao katika misingi ya kiimani na kuwasomesha.**

# Ujenzi wa madarasa watokomeza utoro kwa wanafunzi

**Na Mwandishi wetu,** TABORA

UJENZI wa madarasa katika Shule ya Sekondari Mole wilayani Sikonge mkoani Tabora iliyogharimu Sh. milioni 140 kumesaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa shule hiyo, Bakari Bakari, wakati wa mahafali ya kidato cha nne, kwamba mradi huo ulikamilika mwaka jana umehusisha ujenzi wa madarasa saba, kufanya jumla ya vyumba kuwa 17.

Alisema kwamba awali serikali ilitoa Sh. milioni 80 za Uviko-19, kisha ikaongeza Sh. milioni 60, huku wananchi nao wakichangia nguvu kazi kufanikisha mradi huo.

Alisema vyumba hivyo (17) vina uwezo wa kuchukua wanafunzi 700 na shule kwa sasa ina wanafunzi 405, hivyo uhaba wa madarasa uliokuwapo awali umemalizika.

"Watoto sasa wanajielekeza ipasavyo katika masomo. Mbali na mradi wa madarasa, serikali imefanya maboresho mbalimbali ikiwamo ujenzi wa maabara," alisema na kuongeza:

"Hali ya ufaulu wa masomo ya sayansi kwa sasa ni nzuri ikilinganishwa na kipindi ambacho shule haikuwa na maabara. Mfano halisi ni kupitia mtihani wa utamilifu mkoa mwaka huu, ambapo ni mwanafunzi wetu pekee aliyepata ufaulu wa alama 'B'. Hii imetupa hata sisi walimu hari kubwa ya kazi," alisema.

Bakari alisema bado wanafunzi wachache wanaendekeza vitendo vya utoro, hivyo akaomba msaada wa vifaa vya michezo ili kuwavutia zaidi kupenda shule.

Naye mgeni rasmi katika mahafali hiyo, Chifu wa Igalula Ugunda (Sikonge), Hamisi Kalimwage, aliahidi kutoa msaada wa kuzuia vitendo vya utoro pamoja na kukuza vipaji vya wanafunzi.

Msaada huo ni kompyuta kwa lengo la kupanua wigo wa masomo kwa vitendo, ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kwenda na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Chifu Kalimwage alisema: "Msaada huu utawafikia mapema sana Desemba mwaka huu. Hilo liko ndani ya uwezo wangu na nitaendelea kuwa karibu na jamii ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi".

ALHAMISI OKTOBA 12, 2023
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

**TFS Sengerema na kampeni kuzalisha miti 200,000 ya kuwagawia wananchi**




Ukurasa 13

**UNFPA inavyopambana kuishika mkono serikali udhibiti wa mimba**




MAZINGIRA

VILIO MAJI, BARABARA, ARDHI KATAVI...

# Kitimoto cha Chongolo, kila waziri 'ajikaanga' anavyotimiza ahadi ya Rais

• Awaanika mkutano umma watoe majibu

**Neema Hussein,** MPANDA

***JANA sehemu ya kwanza ya makala, ilikuwa na simulizi ya ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, mkoani Katavi, kukagua miradi na hali ya wananchi kuhusiana na ilani ya uchaguzi ya chama chake. Vilio vilivyojitokeza ni vya maji, ardhi, barabara na afya. Siku ya mwisho mjini Mpanda, akawawajibisha kujieleza kwa umma namna wanavyotekeleza ahadi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan mkoani Katavi. Fuatilia...***



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akinadi hoja zake katika mkutano mjini Mpanda, alipoandamana na mawaziri, walitoa majibu ya kero za umma. **PICHA: NEMA HUSSEIN**

KATIKA ziara yake wiki iliyopita, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwenye staili yake ya kupokea sauti ya umma mkoani Katavi, alikomalizia ziara ya siku sita wikiendi iliyopita, akajikuta anapokea mambo makuu manne.

Vilio vya ubovu wa barabara, uhaba wa watumishi afya, migogoro ya ardhi, shida ya maji na umeme.

Akisomewa taarifa ya utekelezaji mradi wa Kituo cha Afya Ikola, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Alex Mrema, anaeleza kituo hicho kimegharimu shilingi milioni 408, ambazo milioni 400 ni mapato ya ndani na milioni nane, ni zao la nguvu za wananchi.

"Mradi huu ulianzishwa ili kukidhi mahitaji ya watu wa Ikola na vijiji jirani kutokana na kutokea mara kwa mara kwa magonjwa ya milipuko.

"Mradi huu unasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupunguza gharama wanazoingia wananchi kwenye kutibiwa Hospitali ya Rufani ya Manispaa ya Mpanda," anasema Dk. Mrema.

Hapo akapokewa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko na viongozi wengine, akiwamo mbunge, wanaomba kituo hicho kiwe hospitali ya wilaya, kutokana na eneo hilo kuwa na magonjwa ya milipuko.

Mkuu wa Mkoa, anasema mapato ya ndani ya halmashauri ya kila mwaka yatachukua muda mrefu kukamilisha mchakato wa kukifanya kituo hicho kuwa hospitali teule ya wilaya, hivyo anaomba usaidizi wa kiserikali wa fedha kutoka serikali kuu.

Mbunge wa Mpanda Vijijini, Seleman Kakoso, anaiomba serikali kuongeza idadi ya watumishi wa afya katika vituo vya afya wilayani humo, ili huduma iendane na uzuri wa majengo yalivyopo na wingi wa hospitali hizo.

Pia wakazi nao wakatoa shukurani kutoka kwa wakazi kwa serikali, kufanikisha ujenzi wa kituo hicho, wakinena inawapunguzia safari ndefu kufuata matibabu.

**KAULI YA CHONGOLO**

Hapo Chongolo akawaahidi kufanyia kazi maombi hayo, akiwasisitiza wajawazito kujifungulia katika vituo vya afya, kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Anasema, takwimu zinaonyesha vifo vya wajawazito wilayani Tanganyika, zaidi vinatokana na kinamama kujifungulia majumbani.

"Lengo la serikali kusogeza huduma hizi ni kumlinda mama, tunapata vifo vya mama na mtoto, ambavyo vinaepukika," anatamka Chongolo na kuendelea:

"Vingi vinatokana na kinamama kujifungua kwa njia ya kienyeji, achaneni na mila hizo, nendeni kwenye vituo vya afya na hospitali zetu."

Pia anaahidi ujenzi wa barabara ya kutoka Kagwila kwenda Karema, akitaka ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, ili Bandari ya Karema ianze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Ni hoja yake akiwa wilayani Mpimbwe, akakutana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dk.Samia.

Katibu Mkuu wa CCM, anaonyesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa barabara inayotoka Kibaoni kuelekea Stalike, inayojengwa kwa kiwango cha lami.

Hiyo inayomfanya atoe ahadi kwa wananchi ya kumwita Waziri wa Ujenzi, pindi atakapohitimisha ziara yake, ili azungumze na makandarasi wanaotekeleza mradi huo, kisha kutoa majibu ya uhakika kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

INAENDELEA UK.12

MAZINGIRA

# Kitimoto cha Chongolo, kila waziri 'ajikaanga' anavyotimiza ahadi ya Rais



Umati uliokusanyika kumsikiliza. **PICHA: NEMA HUSSEIN**

**INATOKA UK.11**

Chongolo anasema, serikali ikishapitisha fedha na kuzitenga kwa ajili ya mradi, matamanio ya CCM ni kuona mabadiliko yakionekana kwenye mradi.

"Barabara hii ni kubwa ina umuhimu mkubwa kiuchumi watu huku mnajishughulisha kwa dhati na shughuli za kilimo na maendeleo mnachotaka ni barabara nzuri kwa ajili ya kusafirisha mazao yenu kwenda kwenye masoko," anasema Chongolo.

**WILAYANI MLELE & NSIMBO**

Wilayani Mlele, akatembelea Bwawa la Maji Nsekwa linalojengwa kwa ajili ya kutunza na kuhifadhi maji ya mvua, ili kumaliza changamoto ya maji katika eneo hilo.

Chongolo anasema, maelekezo ya chama hicho ni kuhakikisha wanajenga mabwawa mengi ya kuhifadhi maji ya mvua, ili kutatua changamoto ya maji nchini.

Hapo anatoa wito kwa halmashauri kutenga eneo kubwa kwa ajili ya matumizi ya wananchi ili kuzuia shughuli za kibinadamu kufanyika pembezoni mwa bwawa hilo.

Akisoma taarifa ya utekelezaji mradi wa bwawa hilo, Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Mhandisi Charles Mengo, anasema ni mradi unaotarajiwa kuboresha upatikanaji wa majisafi na salama kwa vijiji 16.

> **Maelekezo ya Rais ni ni kwamba barabara hiyo ijengwe haraka iwezekanavyo, ili bandari iweze kufanya kazi hivyo tuko kwenye hatua za mwisho za ununuzi.**

Hoja ya Maji ikajitokeza tena katika Kata ya Ugala, Halmashauri ya Nsimbo, baada ya wananchi kulalamika kuliwa na mamba wanapoenda kuchota maji mto Ugala.

Hapo Chongolo akabeba dhamana ya kuahidi mabadiliko katika mradi wa maji Katambike, ambao umechelewa kukamilika kutokana na mkandarasi husika kufariki. Chongolo anafafanua: "Dhamana hii ni kubwa dhamana hii inatutaka tubebe dhamira ya dhati ya kutekeleza hayo ndani ya mioyo yetu."

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Meneja RUWASA Wilaya ya Mpanda, Christian Mpena, anasema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 25 na utakapokamilika utawanufaisha wananchi zaidi ya 12,000, kupunguza madhila anayolalamika mwananchi kwa sasa.

Anasema ujenzi wa mradi ulianza kutekelezwa Juni 21 mwaka jana, ukitarajiwa kukamilika Desemba, lakini mkandarasi ameongezwa muda mpaka tarehe 30, mwezi huu, mradi ukigharimu zaidi ya shilingi milioni 700.

Pia Chongolo akatembelea na kukagua Skimu ya Umwagiliaji Ugala, akikiri umekwama tangu mwaka 2007 na kuahidi kuweka mipango ya kuukwamua.

**SHIDA YA ARDHI**

Akiwa katika eneo hilo Mbunge wa Jimbo la Katavi, Issack Kamwelwe, alimwomba Katibu Mkuu kulichukua suala la migogoro ya mipaka ya vijiji baina ya serikali na wananchi, kwamba ni kubwa.

Mbunge akalalamika: "Mipaka ya vijiji iliwekwa mwaka 1954, eti hiyo ndio tuendelee kuwa nayo, matokeo yake wananchi walijiongeza, wakavamia na msitu wa kijiji wakaweka mashamba na wameendelea kulima zaidi ya miaka 15."

Anaendelea: "Juzi serikali imekuja kuweka mipaka katikati ya mashamba wanayoyalima na kutuleta changamoto kubwa sana."

Katika hilo, Chongolo akalitolea ufafanuzi kwamba: "Siwezi kutolea kauli suala linalohusu ardhi, kwa sababu sio mtaalamu wa ardhi, lakini nina watalaamu wa ardhi wakianza na Waziri wa Ardhi na timu ya wataalamu msululu.

"Chini yake tutaenda kuzungumza na nimewambia tarehe 7(wikiendi iliyopita ) tutafanya mkutano mkubwa pale Mpanda Mjini, kwenye ule mkutano nitawaita baadhi ya mawaziri waje watoe ufafanuzi wa mambo ambayo tumeyakuta kama changamoto kwa wananchi huku.

"Lakini, watueleze na mpango wa kutatua hizo changamoto," akatamka Chongolo wakati akimjibu mbunge huyo.

**UFAFANUZI WA JUMLA**

Majibu ya jumla kutoka kwa mawaziri katika mkutano mkubwa wa hadhara uliofanyika Mjini Mpanda katika viwanja vya Shule ya Msingi Kashato, akianza na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Slaa.

Hapo akafafanua Wizara ya Ardhi imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995, ikiundwa upya kupata inayoendana na hali ya sasa nchini.

Ziara ya Katibu Mkuu Chongolo, ilibaini mapungufu mbalimbali ya ardhi ikiwamo Sheria za Ardhi ya Mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji, pamoja na nyinginezo zinazosimamia sekta ya ardhi.

Waziri Slaa anasema, sera hiyo inapokamilika itamsaidia Mtanzania, akiwamo wa mkoani Katavi.

Silaa anasema, Sheria ya Vijiji ya Mwaka 1999 ilitungwa kwa nia njema, lakini iliweka mamlaka ya ardhi ya vijiji mikononi kwa wananchi, ikitoa nguvu kwa viongozi wa vijiji kupitia halmashauri kuu na mikutano mikuu ya vijiji kutoa ardhi.

Anasema kuna viongozi wa vijiji wanaofanya vizuri, lakini wengine wanapotosha, hata kusababisha migogoro vijijini, akitaja waathirikaji wakubwa ni wananchi kwa makosa anayoyafanya mwenyekiti wa kijiji kwa maslahi yake.

Pia Naibu Waziri wa Ujenzi, akawa na ufafanuzi: "Barabara ya Kagwila, Kasekese hadi Karema yenye kliomita 112, tunajua uwekezaji mkubwa uliowekwa kwenye Bandari ya Karema.

"Maelekezo ya Rais ni ni kwamba barabara hiyo ijengwe haraka iwezekanavyo, ili bandari iweze kufanya kazi hivyo tuko kwenye hatua za mwisho za ununuzi."

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, anayefafanua: "Niwahakikishie wana - Katavi na nikuhakikishie Katibu Mkuu, sisi Wizara ya Nishati hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha wana - Katavi wanapata umeme wa uhakika.

"Ahadi yetu tuliyoitoa kuunganisha mkoa huu na umeme wa Gridi ya Taifa ifikapo Juni 2024 iko palepale hatutaongeza muda; dakika, siku, mwezi wala mwaka."

Ilipofika zamu ya Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akawa na ufafanuzi wenye kauli: "Eneo la Ugala nianze nalo ndugu Katibu Mkuu, maelekezo yako nimeyapokea. Hii Wizara ya Maji sio ya kuchezewa, kesho asubuhi nitakua Ugala.

"Leo nalala nawaza Ugala, mkandarasi ambaye anakuwa legelege hafanyi kazi kwa kufuata mkataba, hafuati maelekezo yetu 'tutamla kichwa' kesho. Nafanya maamuzi kwa niaba ya waziri wangu (Jumaa Aweso)."

Baada ya majibu hayo, Katibu Mkuu Chongolo, akasisitiza dhamira ya CCM, kuletea maendeleo na kutatua changamoto na migogoro inayoepukika, ikiwamo kutekeleza kila kitu kilichoahidiwa kwenye ilani.

AFYA

# UNFPA inavyopambana kuishika mkono serikali udhibiti wa mimba

## • MSD yakabidhiwa vifaa vya mamilioni

**Na Yasmine Protace**

UZAZI wa mpango kitaalamu, ni taarifa, njia na mbinu zinazoruhusu watu binafsi kuamua kama na lini wapate watoto; hiyo ni pamoja na njia mbalimbali zinazopaswa kutumika.

Hapo kunatajwa tembe, vipandikizi, vifaa vya ndani ya mfumo wa uzazi na upasuaji, vyote ni huzuia uwezo wa kushika mimba. Pia, kuna njia za vizuizi kama za kondomu na matumizi ya kalenda kwa mwanamke kujizuia na mimba.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Idadi ya Watu (UNFPA) nchini Tanzania, Mark Bryan Schreiner, akatamka kuwa kila mwaka ifikapo Septemba 26 ni Siku ya Kuzuia Mimba Duniani.

Ni kauli yake katika makabidhiano ya ishara hivi karibuni, katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Dar es Salaam, ambako UNFPA wakathimisha ununuzi wa bidhaa za afya ya uzazi zenye thamani ya mamilioni ya Dola za Marekani 9,519,235, (Sawa na shilingi 23,893,289,369.24), kati yake Dola milioni 7,528,909 zimetoka kwa UNFPA na Dola 1,990,326 kutoka Taasisi Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza.

Anasema kuwa, bidhaa hizo zilinunuliwa uanzia Julai 2022 hadi sasa na kutoa vidhibiti mimba vya kutosha vya kisasa kutosheleza mahitaji ya wanandoa milioni tatu kwa mwaka mmoja.

Anasema kutokana na ununuzi huo, walizuia makadirio ya mimba zisizotarajiwa 1,473,532; vifo vya uzazi 1,958; na utoaji mimba usio salama 400,620, katika huduma ya afya ya moja kwa moja.

Pia, anataja mafanikio hayo yanawezekana tu, kwa ushirikiano wao wa muda mrefu na serikali ya Tanzania.

Mark anasema uzazi wa mpango ni taarifa, njia na mbinu zinazoruhusu watu binafsi kuamua kama na lini wapate watoto.

"Hii ni pamoja na njia mbalimbali za uzazi wa mpango ikiwa ni pamoja na tembe, vipandikizi, vifaa vya ndani ya uterasi, taratibu za upasuaji ambazo huzuia uwezo wa kuzaa, na njia za vizuizi kama vile kondomu - pamoja na mbinu zisizo vamizi kama vile njia ya kalenda na kujizuia," anasema.

Anafafanua kuwa, kupanga uzazi kunajumuisha habari za jinsi ya kupata mimba inapohitajika, na matibabu ya utasa, akinena UNFPA inaunga mkono vipengele vingi vya upangaji uzazi wa hiari.

Hapo anataja ni pamoja na kununua vidhibiti mimba, kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya




Mwakilishi wa UNFPA nchini, Mark Bryan Schreiber, akizungumzia baada ya kukabidhi vifaa vya uzazi wa mpango kwa serikali Tanzania. **PICHA ZOTE: YASMINE PRIOTACE**




Baadhi ya vifaa vya uzazi wa mpango vilivyokabidhiwa kwa serikali, vikitolewa na Ubalozi wa Uingereza nchini na UNFPA, Ofisi ya Tanzania.

kuwashauri watu binafsi kwa usahihi na kwa umakinifu kuhusu chaguzi zao za kupanga uzazi na kukuza elimu ya kina ya kujamiiana shuleni.

Mark anaongeza kuwa, upatikanaji taarifa za uzazi wa mpango, ni muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia, kwani wakati wanawake na wanandoa wanawezeshwa kupanga namna ya kupata watoto, na wangapi, ni vyema elimu hiyo ikasambazwa

"Hii inaimarisha usalama wao wa kiuchumi na ustawi wao na wa familia zao," anasema, akifafanua kuwa faida hizo huchangia kupunguza umaskini na maendeleo ya kimataifa.

### SAFARI NCHI IEBNDAKO

"Ni manufaa yaliyotambuliwa katika Mpango wa Utekelezaji wa Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo (ICPD), akiutaja mkataba unaoweka msingi wa kazi nyingi za UNFPA kwa matamshi:

"Haki ya wanaume na wanawake kufahamishwa na kupata njia salama, zenye ufanisi, nafuu na zinazokubalika za kupanga uzazi, kwa chaguo lao."

> **Kutoa taarifa na huduma za upangaji uzazi ni sehemu muhimu ya juhudi hizi. Ulimwengu unapobadilika kote kote, kufikia ufikiaji wa upangaji uzazi kwa watu wote huchukua uharaka mpya.**

Mark anaongeza kuwa, uzazi wa mpango pia unaweza kusaidia nchi kutambua idadi ya watu inayotaka hata ikaipunguza idadi ya wategemezi.

Anasema UNFPA ni mshirika mkuu katika ushirikiano wa kimataifa wa Mpango wa Uzazi (Family Planning) wa 2030, unaolenga kuwa wa hiari na kisasa kwa anayeutaka.

Mark anasema, inachangia katika siku zijazo wanawake na wasichana kila mahali kuwa na uhuru wa kuishi maisha yenye afya, kuamua wenyewe kuhusu kutumia uzazi wa mpango na kupata watoto, hata wakashiriki sawa katika jamii na maendeleo yao.

"Tunaipongeza Serikali ya Tanzania kwa dhamira ya FP2030 ya kuendeleza uzazi wa mpango unaozingatia haki, na ongezeko lililopangwa la asilimia 10 kila mwaka, katika mgawo wa sasa wa shilingi bilioni 14 za Tanzania zitakazotolewa kikamilifu kwa ajili ya ununuzi wa vidhibiti mimba.

"Kupitia Ushirikiano wa UNFPA wa Ugavi, tunatazamia kushirikiana zaidi na Serikali ya Tanzania ili kuendelea na utekelezaji wa makubaliano ya kimkataba ya nchi hiyo yaliyotiwa saini Desemba 2022 na kuimarisha dhamira yetu ya pamoja ya ufadhili," anasema.

Anaongeza kuwa ni hatua muhimu na nchini, huku UNFPA ikilenga kufikia matokeo matatu yenye mabadiliko makubwa duniani: Kukomesha vifo vya uzazi; kukomesha hitaji lisilotimizwa la upangaji uzazi; na kukomesha unyanyasaji wa kijinsia na mazoea hatari.

Mark anaendelea: Kutoa taarifa na huduma za upangaji uzazi ni sehemu muhimu ya juhudi hizi. Ulimwengu unapobadilika kote kote, kufikia ufikiaji wa upangaji uzazi kwa watu wote huchukua uharaka mpya."

Anasema mkakati wa UNFPA wa Upangaji Uzazi, 2022-2030, ni wito wa kuchukua hatua umuhimu wa upangaji uzazi na nguvu zake za mabadiliko katika ulimwengu tofauti na unaobadilika.

Anasema UNFPA inasisitiza dhamira yake ya kuendelea na kipunga mkono serikali nchini kupitia Wizara ya Afya, katika kuimarisha mfumo wa afya ili kukabiliana na mahitaji ya afya ya ujinsia na uzazi, hasa ya wanawake na wasichana.

Mark anataja juhudi hizo, inajumuisha kuimarisha usimamizi wa mnyororo wa ugavi na kuendelea kusaidia kujenga uwezo wa watoa huduma.

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA

# TFS Sengerema na kampeni kuzalisha miti 200,000 ya kuwagawia wananchi

**Na Anthony Gervas,** Sengerema

MISITU ya kupanda asili ni rasilimali inayolinda, kutunza mazingira ikiwemo uoto wa asili, hapa nchini kuna Wakala wa Huduma za Mistu Tanzania(TFS), ambayo ni Sekta Mahsusi iliyoanzishwa na serikali mwaka 2011,kwa ajili ya kuhifadhi Rasilimali Misitu na Nyuki.

Vilevile, kusimamia taratibu za Uvunaji na Usafirishaji wa Mazao ya Mistu na Nyuki,Kazi ya Uhifadhi inajumuisha misitu ya kupandwa na asili kwa kufuata usimamizi wa Sheria za Nchi za mwaka 2002 namba 14 ndiyo inayotumika.

TFS imegawanyika katika kanda mbalimbali ikiwemo kanda ya Ziwa, Mkoa wa Mwanza ndiyo kitovu chake kikuu cha usimamizi kanda ya ziwa,uhamasishaji wa suala zima la utunzaji wa mazingira jamii katika maeneo yanayozunguka hifadhi za mistu ya kupandwa na asili nalo ni miongoni mwa majukumu yao.

Mifugo na Kilimo ni mambo mojawapo yanayotajwa kuwa sehemu ya uharibifu wa mazingira katika Ikolojia ya Viumbehai na mazingira yake kwenye hifadhi, pia shughuli za kibinadamu zinafanywa na wananchi wanaozunguka maeneo hayo ili kufikia malengo waliyokusudia.

Katika wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza,TFS inapambana kuhakikisha wilaya hiyo,inakuwa ya kijani msimu wote wa kiangazi na masika, kuhamasisha wananchi kupanda miti na kugawa miche bure kwenye taasisi mbalimbali, ni mambo muhimu yanayofanywa na wakala huo.




Mhifadhi wa Huduma za Misitu Wilaya ya Sengerema(TFS) James Aloyce. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

### MHIFADHI MISITU

Mhifadhi Misitu Wilaya ya Sengerema, James Aloyce, anasema wanakusudia kuzalisha miche ya miti aina mbalimbali, ikiwamo ya mbao, nguzo na kivuli, hivi wakiwa wamezalisha miche ya kivuli aina ya Senasi na miche 30,000 ya Misindano (Mikalebea) itakayogawiwa bure kwenye taasisi za serikali, binafsi na wananchi.

Anataja mwaka uliopita 2021, taasisi mchanganyiko ziligawiwa miche bure ambazo ni shule za sekondari 20 na msingi 82, pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) halmashauri ya wilaya hiyo, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mshauri wa Mgambo, Taasisi za Dini pamoja na Mamlaka ya Maji Sengerema (SEUWASA)

Mwaka huo TFS ilikuwa na lengo la kugawa miche 100,000 lakini ilivuka malengo na kugawa miche 133,880 katika taasisi kiserikali na binafsi, huku mwaka huu 2023/24 imejipanga kugawa miche 200,000, ambayo ni miti ya mbao, vivuli na nguzo, lengo kila mwaka kuzalisha miche 100,000.

Mhifadhi Aloyce anasema, moja ya kazi ya kuandaa uzalishaji au uoteshaji wa miche kwenye viriba katika vitalu, uandaaji unaotumia udongo wa mlimani, ukichanganywa na pumba laini za mpunga zilizooza ambazo zimekaa miezi miwili na kugeuka kuwa mbolea.

Anataja uchanganyaji wake hutumia vipimo, udongo huo na mbolea ya mpunga, akitaja gharama za kuupata udongo ni shilingi 70,000 kwa tripu moja ya gari na pumba shilingi 30,000, wakitumia bajaji na udongo unapoadimika, wanafuata umbali wa kilomita saba.

Wilaya ya Sengerema ina misitu ya asili Kisiwa cha Maisome chenye ukubwa wa hekta 9,319.238 na Kisiwa cha Kome chenye hekta 2,487, Msitu wa kupandwa wenye ukubwa wa hekta 21,880 ulioko Buhindi, katika Halmashauri Buchosa.

### CHANGAMOTO Z ILIZOKO

Mhifadhi huyo anataja ni katika usimamizi mgumu wa jamii wanapopewa miti ya kupanda, mingi hunyauka kwa jua kutokana na utunzaji duni, pia kutotambua ardhi sahihi ya kupanda aina ya miche aliyopewa, ikiwamo ya mbao, vivuli na nguzo.

Lingine analitaja, ni kutozingatia kanuni na kalenda ya miezi ya kupandia miti, ambayo ni kuanzia mwezi Novemba hadi Machi, msimu wa mvua nyingi.

Pia, anasema haja ya kupanda miti kitaalaamu, kutobaini maeneo yenye ukame mkubwa ambayo mimea haikui, pamoja na udongo unaofaa kulingana na miti husika.

Anasema, lengo la TFS Sengerema ni kuungana na wananchi, kuendeleza utalii wa ndani wa kiikolojia, ili kutengeneza boti za kuvulia samaki au wakati wa utalii ziwani, katika Kisiwa cha Kome, ili kuongeza mapato ya serikali, watalii wanapotembelea kisiwani humo.

Faida mojawapo za miti ya asili inatajwa kuwa ni kuyafanya mazingira kuwa bora, hali ya hewa kuwa nzuri, kulinda vyanzo vya maji, kuongeza vipato vya wananchi na kupata mbao, kuni, mkaa na kutengeneza vitu mbalimbali vya thamani kulingana na ubora wake.

### MIKAKATI KIWILAYA.

Aloyce anasema, walio nao ni Sengerema, ni kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya uhifadhi misitu aina zote na madhara yake, kuendelea kusaidia jamii kuiwezesha inayozunguka maeneo ya hifadhi za Mistu.

Anajinasibu kwamba, mwaka huu wanatarajia kuzipa msaada wa madawati 100 shule za msingi,katika kata za Buhama na Maisome kila moja madawati 50,huku akisema elimu ya uhifadhi itaendelea kutolewa ngazi ya vijiji vinavyopakana na maeneo husika na kugawiwa miche bure ya kupanda.

Mkakati mwingine ni kuendelea kudhibiti ukataji ovyo wa miti kwenye Hifadhi zao, uharibifu wa mazingira utokanao na Mifugo, Kilimo, kuwapa elimu jamii juu ya kutengeneza mashamba darasa ya miti ya kupanda ili kuepuka uharibifu mazingira ili wilaya iendelee kuwa ya kijani.

Anawataka wananchi kulinda vyanzo vya maji kwa kupanda miti kwa wingi, ili kupunguza mmomonyoko wa udongo, akisisitiza kuvuna iti iliyofikia umri wa kitaalam kuvunwa ambayo miaka 18, itakayokuwa na ubora zaidi sababu imekomaa vizuri.

## UNFPA inavyopambana kuishika mkono serikali udhibiti wa mimba

**INATOKA UK.13**

### OFISA WA UINGEREZA

Kemi Williams, Mkurugenzi wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania, anasema wao wamejitolea kusaidia upangaji uzazi wa hiari na kuwezesha watu kupata huduma bora za afya ya ngono na uzazi.

Anasema utoaji wa bidhaa za uzazi wa mpango unahakikisha kuwafikia wanawake wote, bila ya kujali walipo, uwezo au hali ya elimu.

"Uzazi wa mpango ni mojawapo ya vichochezi vya nguvu zaidi vya maendeleo na ustawi. Wakati wanawake na wasichana wanapata fursa ya kupanga uzazi, wanaweza kumaliza elimu yao, kupata ajira na kutimiza malengo yao.

"Hii hufungua ustawi wa kiuchumi katika ngazi ya kitaifa kusaidia kuibuka kwa uchumi na jamii imara. Uingereza inajivunia kuchangia katika kusaidia maendeleo ya uchumi wa Tanzania kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za uzazi wa mpango," anasema.

Anaendelea: " Mpango huu una vipengele vikuu viwili; ununuzi wa bidhaa kupitia UNFPA na) utoaji wa huduma kupitia Engender Health na Marie Stop Tanzania."

Mark anaeleza kuwa, katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji, mpango huu umewafikia wateja wapya nusu milioni kwa njia ya upangaji uzazi watakayochagua, ilitoa ulinzi wa zaidi ya milioni 3.4 wa miaka kwa wateja wapya na wanaorejea na kusaidia kuzuia mamilioni ya mimba zisizotarajiwa na vifo vya kinamama.

Anaongeza kuwa, licha ya maendeleo nchini kuna haja ya Tanzania kufanya juhudi zaidi kuboresha upatikanaji wa afya na huduma kamili za ngono na uzazi.

Anasema mpango wa Uingereza, ni kuongeza matumizi ya uzazi wa mpango, ukilenga vikundi vya umri wa vijana, hasa katijka umri wa kupevuka.



# Kituo cha Maarifa Manyoni chapunguza maambukizi VVU

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

IMEELEZWA kuwa Kituo cha Maarifa cha Manyoni ambacho kimejengwa kando ya barabara yanapoegeshwa magari ya masafa marefu, kimechangia kutoa elimu ya kupunguza ongezeko la maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa makundi hatarishi.

Akitoa taarifa jana wilayani hapa kwa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi ilipotembelea kituo hicho, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk.Furaha Mwakafwila, alisema kituo hicho kilijengwa na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kwa kushirikiana na mgodi wa Geita Gold Mining ikiwa ni moja ya jitihada za serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kupambana na maambukizi mapya ya VVU.

Alisema lengo ni kutoa huduma kwa madereva wa masafa marefu, wasafiri wanaotumia Barabara ya Dar es Salaam-Tabora -Singida pamoja na watu wote wanaoishi Manyoni.

Alifafanua kuwa katika huduma ya upimaji wa VVU kuanzia mwaka 2022 hadi 2023 watu 1990 wamepima afya zao ikiwamo madereva ni 684.

Alisema kati ya watu hao waliopimwa afya 19 waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kuunganishwa katika kliniki za tiba na matunzo.

"Kituo hiki kimekuwa muhimu katika utoaji huduma za afya kwa wananchi wanaozunguka katika eneo hilo ndio imekuwa zahanati yao kuu ya kupata huduma zote," alisema.

Alibainisha baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa kituoni hapo kuwa ni kuongezeka kwa wateja wanaokuja kupata huduma za ushauri nasaha na kupima afya zao.

Naye, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, aliwaasa wananchi wa Manyoni kufika kwenye kituo hicho kupata huduma zinazotolewa huku wabunge wakihamasisha wananchi kupima afya zao.

# Uhaba wa maji, ukosefu wa majosho vyawatesa wafugaji

**Na Paul Mabeja,**
MANYONI

WAFUGAJI wilayani Manyoni mkoani Singida wamelalamikia uhaba wa huduma za maji na majosho kwa ajili ya mifugo yao, hali ambayo inachangia kupunguza tija katika sekta hiyo nchini.

Rock Vicent, mmoja wa wafugaji hao akizungumza na waandishi wa habari jana wilayani hapa, alisema kukosekana kwa huduma za majosho kwa ajili ya kuogeshea mifugo kunachangia kupunguza thamani ya mifugo yao.

Vicent, alisema kukosekana kwa majosho mifugo yao imekuwa ikikabiliwa na magonjwa mbalimbali hali ambayo inapunguza bei na wakati mwingine kukosa soko kabisa na kusababisha jamii za wafugaji kuendelea kuwa maskini.

"Josho ambalo tunalitegemea ni moja ambapo kama tutahitaji kupeleka mifugo yetu kwa ajili ya kuogesha dawa tunalazimika kutembea zaidi ya saa tatu na mifugo yetu hali ambayo inasababisha wakati mwingine kukosa muda wa kuwapa malisho wanyama wetu "alisema.

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo wafugaji walilazimika kuchangishana fedha kwa ajili ya kuanza kujenga josho la kuogeshea dawa mifugo yao.

"Tumechangishana fedha tukaanza ujenzi lakini hadi sasa mchanga na nondo tulizonunua zinaozea pale kwani fedha ambayo serikali ilipaswa kutupatia viongozi wameshindwa kuifuatilia.

"Mbunge wetu alituambia kuwa katika ujenzi wa josho serikali tayari imetoa shilingi milioni 18 lakini hadi sasa hatujaona kitu, tunaimba serikali kutusaidia katika hili ili tupate josho na kuondokana na adha hii"alisisitiza.

Alisema hali hiyo kama isipofanyiwa kazi kwa muda mrefu itawaumiza wafugaji kwakuwa uwekezaji wao katika sekta ya mifugo hautakuwa na tija kwao na taifa kwa ujumla.

"Mifugo yetu hivi sasa inakosa soko minadani kutokana na kukosa ubora kutokana na kukosa huduma za josho kwa ajili ya dawa, maji ya uhakika lakini pia malisho ni shida" alisema.

Pascal Mbiya, alisema katika kata yao ya Chikuyu wilayani hapa, migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kiasi kikubwa inachangiwa na maji.

Alisema eneo ambalo wanalitegemea kwa ajili ya kunywesha mifugo yao wakulima pia wamelima bustani zao, hivyo kuwa moja ya sababu ya migogoro baina ya jamii hizo mbili.

Kaimu Katibu wa Chama cha Wafugaji (CCWT), Kanda ya kati Simon Ndaki, alisema moja ya sababu zinazokwamisha juhudi za wafugaji nchini ni viongozi kutozingatia maagizo ya viongozi wa ngazi za kitaifa.

Katibu wa Kamati ya Uchumi, Mipango na Fedha wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT)alikiri kuwa moja kati ya kero kwa wafugaji katika wilaya hiyo ni majosho.

Alisema tayari wameshaongeza na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambayo tayari imeshatoa Sh.milioni 18 kwa ajili ya ujenzi wa josho litakalo ondoa adha hiyo kwa wafugaji.

Alisema: "Tayari serikali ilishatoa kiasi cha Sh. milioni 18 kwa ajili ya ujenzi wa josho la mifugo shida nadhani ni uongozi tuu umeshindwa kuzifuatilia fedha hizo lakini tayari zilishatolewa".




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania ambaye pia ni Mkurugenzi wa Tehama, Jema Msuya akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la benki hiyo, mjini Mpwapwa mkoani Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BMH kuanzisha upasuaji moyo bila kufungua kifua

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HOSPITALI ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH) imesema kuanzia Oktoba 16, mwaka huu itaanza kutoa huduma ya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua kwa watu wazima.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika alisema lengo la kuanza kutoa huduma hiyo ni kuipunguzia mzigo Taasisi ya Matibabu ya Moyo ya Jakaya Kikwete ambayo kwa sasa inapokea wagonjwa kutoka sehemu mbalimbali nchini.

"Kambi ya madaktari bingwa inatarajia kuanza Oktoba 16 mwaka huu hapa hospitalini, awali hospitali ilikuwa ikitoa matibabu haya kwa watoto wadogo na kuwapa rufaa watu wazima kwenda Jakaya Kikwete," alisema.

Alisema hospitali hiyo imeamua kuanzisha matibabu ya aina hiyo ili kuokoa maisha ya watu wenye tatizo hilo ili kuwapunguzia gharama wananchi kutoka Dodoma kwenda Dar es salaam lakini na kuipunguzia msongamano Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Hata hivyo alisisitiza zaidi ya kuwa matibabu ya moyo ya aina zote yataendelea kutolewa katika hospitali hiyo kwa wagonjwa ambao watajitokeza kupata huduma hiyo.

Akizungumza kuhusu miaka nane tangu kuanzishwa kwa hospitali hiyo, Dk. Chandika alisema hospitali hiyo imepata mafanikio makubwa, ikiwamo kuanzishwa kwa huduma za utoaji matibabu ya magonjwa mbalimbali ambayo awali wagonjwa walikuwa wakipewa rufaa kwenda nje ya nchi.

Alibainisha kuwa zaidi ya wagonjwa 100 wamepata huduma ya kubadilishwa viungo na kuwekea bandia hususani wenye matatizo ya magoti na miguu.

Akizungumzia ushindi wa tuzo ya daktari bora wa mwaka iliyotolewa kwa Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mifumo ya Damu hususani suala la upandikazaji uloto, Dk. Stella Malangahe alisema umeipa heshima kubwa hospitali hiyo na kuishukuru serikali kutokana na kuwekeza katika sekta ya afya.

"Nawaomba madaktari kuzidi kufanya kazi kwa bidii ili kuifanya BMH kuwa kinara wa matibabu ya afya nchini," alisema.

Kadhalika, alimpongeza Dk. Malangahe na kwamba tuzo hiyo ni ya kitengo chake kutokana na ushirikiano walioufanya kwenye utoaji tiba wa matibabu ya upandikizaji uloto.

Alisema: "Naishukuru sana serikali kwa ujumla kutokana na kuwekeza katika suala la sekta ya afya, huduma hizi bora zinakuja kutokana na vifaa vya matibabu vinavyotolewa katika hospitali mbalimbali hapa nchini".



# Polisi yatumia mabomu, risasi kutawanya wananchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya juzi lililazimika kutumia mabomu ya machozi na risasi za moto kuwatawanya wakazi wa Mtaa wa Gombe katika Kata ya Itezi jijini Mbeya ambao walikuwa wanawazuia mgambo wa jiji kutekeleza amri ya Mahakama ya kubomoa makazi yao.

Wananchi hao wana mgogoro wa ardhi na Kampuni ya S.H. Amon ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 15, ambapo walifikishana katika Mahakama ya Ardhi mkoani Mbeya.

Hivi karibuni ilitoka hukumu ambayo iliwanyima ushindi wananchi hao na kutoa amri ya nyumba zilizojengwa kwenye eneo hilo pamoja na mali za wananchi kuondolewa ili kampuni hiyo ya S.H. Amon ambayo inamilikiwa na aliyekuwa Mbunge wa Rungwe, Sauli Amon iendelee na kazi zake.

Utekelezaji wa amri hiyo ulianza juzi ambapo mgambo wa Jiji la Mbeya pamoja na baadhi ya vijana waliingia katika eneo hilo wakiwa na mashine za kukatia miti na kuanza kuangusha miti ya wananchi, huku wakiwa wamesimamiwa na maofisa wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU).

Baada ya miti kuanza kufyekwa, wananchi hao walianza kutumia silaha za jadi kuwatishia mgambo hao wakiwataka kuacha kufanya kazi hiyo hali iliyowalazimu maofisa wa Jeshi la Polisi kufyatua mabomu ya machozi na risasi za moto ili kuwatawanya wananchi hao.

Hata hivyo wananchi hao waliondoka katika eneo hilo na kwenda kufunga Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kwa kutumia mawe, magogo na magurudumu kabla ya kutawanywa tena na askari.

Mmoja wa wananchi hao, Alex Jackson alisema mgogoro huo awali ulikuwa unawahusu watu watano pekee na kwamba ndio waliopelekwa mahakamani lakini baada ya hukumu kutolewa na wao wanatakiwa kuondoka.

Alisema kuna wakati walikuwa wanazuiliwa kulima wala kukata miti yao kwa ajili ya kuni jambo ambalo lilianza kuwatia wasiwasi na wakaomba waunganishwe kwenye kesi hiyo wakakataliwa. "Tulikataliwa kuunganishwa kwenye hiyo kesi lakini sasa hivi wanataka tuondoke, tunajiuliza kwamba wametukuta wapi wakati awali walitukataa?" alihoji Alex.

Fausta Mboyamwene alisema nyumba yake ambayo anaishi haikuwamo kwenye mgogoro lakini sasa hivi wameunganishwa jambo ambalo linawashangaza na kwamba kuvunja nyumba zao ni hasara.

Alisema hali hiyo ndiyo iliyosababisha waungane na kuzuia mali zao kuharibiwa na migambo hao wa jiji waliokuwa wanafyeka miti na kutaka kubomoa nyumba.

Diwani wa Kata ya Itezi, Sambue Shitambala, alisema utekelezaji wa hukumu ya Mahakama ulianza wakati wananchi walioshindwa kesi hiyo wako kwenye harakati za kukata rufani.

Alisema kesi hiyo ilikuwa inawahusu wananchi watano lakini utekelezaji wa hukumu unawahusu zaidi ya wananchi 150 wa mtaa huo ambao wengi wapo kwenye eneo hilo hata kabla ya mgogoro kuibuka.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema baada ya kutokea vurugu hizo aliamua kusitisha ukataji wa miti na uvunjaji wa nyumba ili kutafuta mwafaka.

Alisema uhalisia unaonyesha kwamba wananchi hao walishindwa kesi mahakamani na kilichokuwa kinafuata ni utekelezaji wa hukumu lakini kwa sasa wanataka kujaribu kufanya mazungumzo na mwenye eneo.

# Uwekezaji tata Chunya waiibua NEMC ikigundua 'madudu' mradi wa mgodi

Inatoka Ukurasa 4

tika harakati za kuuza mradi na kuondoka nchini, Dk. Gwamaka anaendelea: "Tuliona kulikuwa na bwawa la tope sumu ambalo halikuwa limekarabatiwa na maji yakawa yanavuja, yanakwenda kwenye mazingira.

"Na tuliona vilevile maeneo mbalimbali ambayo ni mashimo hayakurejeshwa katika hali iliyopaswa kufanyika."

Dk. Gwamaka anadokeza kuna maswali ya msingi toka NEMC ambayo Sunshine haijayajibu ikiwamo mpango wake wa kuyarejesha mazingira katika uhalisia. Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, sheria inaipa serikali mbadala wa kufanya tathmini ya gharama za kurejesha mazingira hayo na aliyeharibu anatozwa gharama husika na njia mojawapo ni mali za aliyeharibu kuuzwa ili kufidia kiasi kinachotakiwa.

"Tumekwishapata consultant (mtaalamu elekezi), ndiye ambaye anafanya tathmini ya kujua ni kiwango gani," anatamka Dk. Gwamaka akisema uhalali wa kuuza vifaa vya mwekezaji hupewa baraka na mahakama.

Mkurugenzi huyo anasema kemikali za migodini ni hatari kwa afya ya binadamu na wanyama wengine kwa kuwa ni vyanzo vya maradhi kama vile saratani, moyo na figo.

"Ukienda kwenye mazingira, nenda Sunshine, utakuta mazingira yanajieleza. Kwahiyo, mambo kama hayo ambapo mgodi unakuwa umemaliza shughuli zake, ni lazima kuwe na mpango wa urejeshaji mazingira ambao utafanya maisha yawe endelevu. Ni lazima uwapo na uandikwe kabla hata kuchimba mashapu kwenye migodi hiyo.

"Sunshine walitaka 'kulala mbele' (kuondoka) na ndio maana tumeweza kuwadhibiti mapema. Kuna mtambo wao mkubwa tu wa thamani kubwa upo pale. Kwahiyo na wenyewe tumeushikilia.

"Tumekwishawasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya na kulipeleka suala hili kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuhakikisha ule mradi isitokee mtu akaununua bila wilaya, NEMC, Mkuu wa Mkoa kuwa na taarifa," anasema Dk. Gwamaka na kubainisha wanaandaa ripoti kamili kuhusu vipimo vya sampuli walizochukua toka Sunshine.



Samwel Gwamaka

**OFISA WA MGODI**

Salum Kassimu, Meneja Rasilimali Watu katika Kampuni ya Sunshine Mining (T) Limited, akitoa ufafanuzi kwa mwandishi wa habari hizi, anaanza na historia ya mgodi; kampuni ilisajiliwa mwaka 2012 na kufanya kazi kwa miaka tisa kabla ya kusitisha shughuli zake mwaka 2021.

Anabainisha mgodi una maeneo mawili: Chunya kwenye kinu cha kuzalisha dhahabu na Mbangala mkoani Songwe wanakopata malighafi yanayochenjuliwa Matundasi wilayani Chunya.

"Maisha ya mgodi wetu yalikuwa yanafika mwisho. Kwahiyo, kwa mwekezaji mkubwa unakuwa hauwezi tena ukamlipa, ataendesha kwa hasara.

"Tukaamua sasa kufanya ubadilishaji umiliki ili umilikiwe na mtu ambaye ni mchimbaji wa kati ili aweze kuendesha kwa gharama za kawaida. Kwahiyo, tukafanya utaratibu mzuri, tukabadilisha leseni," anabainisha.

Kassimu anasema NEMC walifika kwenye mradi wao, ikiwa ni sehemu ya utaratibu wao, ndipo wakaibua maswali ya mradi kutofanya kazi, hata wakadai ufafanuzi kisheria.

Katika hilo, Kassimu anataja yaliyoibuliwa na NEMC baada ya ukaguzi ni mabwawa ya tope sumu kuvuja na mpango kazi wa kurejesha mazingira katika uhalisia wake, wakitaka kupewa ufafanuzi ndani ya wiki mbili.

Hata hivyo, ofisa huyo wa mgodi anajitetea kwamba maswali hayo wamepewa na NEMC ilhali hawajarejeshewa majibu ya vipimo vya sampuli zilizochukuliwa na baraza hilo.

"Zilichukuliwa sampuli ndani ya bwawa, nje ya bwawa na sehemu tofauti tofauti, lakini majibu hayakuweza kuja," anatamka.

Anaeleza jinsi wanavyotunza vinavyotiririka, kwamba katika mgodi wao wana mabwawa yanayokinga tope sumu na maji yanayojaa humo hayatoki, bali kuna utaratibu wa kuyahifadhi.

Anataja mkakati unaofuata mgodini, kumeandaliwa mpango kazi wa kuhimili uchafuzi wa mazingira na kufanya maboresho dhidi ya uchakavu anaoutaja unashuhudiwa sasa.

Anaendelea na ufafanuzi: "Katika hizi hoja za NEMC hatujakataa kitu chochote. Ni kweli tulikiri makosa na tukaahidi kubadilika. Pia tupo katika mchakato wa kuhakikisha hili ambalo limejitokeza (uchafuzi mazingira) lisitokee tena."

Kassimu anafafanua kwamba kampuni imeshaajiri mhandisi mazingira, anayefanya maboresho ya kiufundi kurejesha ubora wa mabwawa tajwa na mahitaji mengineyo.

Anakana malalamiko dhidi ya mgodi wake kusababisha vifo vya mifugo, akiwa na utetezi eneo anakotumikia kuna uzio na nje ya uzio kuna wachimbaji wadogo, ambao shughuli zao zimebeba athari hizo.

Kassimu katika hoja ya NEMC kwamba Sunshine inamiliki bwawa la tope sumu lisilo na kibali, pia anakana kwa kauli "ni bwawa la awamu ya pili" ambayo imo katika mpango kazi waliouwasilisha serikalini na wamelijenga katika mpango wa dharura.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kabla ya kusitisha uzalishaji, mgodi ulitoa ajira kwa watu 600, wakiwamo walinzi kutoka Suma JKT. Uzalishaji dhahabu ulikuwa wa wastani wa Kg 85 kwa mwaka (dhahabu hiyo ina thamani ya Dola za Marekani 5,062,579 sawa na Sh. bilioni 12.658).

Kabla ya mazungumzo na uongozi wa kampuni ya Sunshine, mwandishi wa habari hizi alishuhudia mambo makuu matatu katika eneo la mradi huo; raia wawili wa kigeni - Wachina waliotajwa na Meneja Kassimu ni wataalamu wa mazingira, miundombinu ya uzalishaji iliyochakaa na mabwawa ya kuhifadhi tope sumu yaliyochakaa, hususani kapeti la kingo za mabwawa.

Novemba mwaka jana, Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Gaspar Mushi, aliiambia Nipashe kuwa binadamu akila masalia ya kemikali za migodini yanayopatikana katika udongo, maji na vyakula, hupata madhara yanayojumuisha kuugua maradhi ya saratani ya figo, kongosho, ini na damu.

Mushi alisema kama migodi inatumia kemikali aina ya zebaki kuchenjua madini, kemikali hiyo inapoingia kwenye maji ya mito, ziwa au bahari, huwaingia viumbe hai waliomo kama vile samaki ambao wanapoliwa na binadamu wanaweza kupatwa na ugonjwa wa Minamata (kupoteza kumbukumbu na mwili kutetemeka).

"Tumekuwa tunafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi huko wilayani Chunya, tumeona kwa kiasi kikubwa hakuna vifaa vya kisasa vinavyotumika kufanya shughuli za uchenjuaji wa dhahabu.

"Athari zinazoweza kujitokeza kwa watu wanaokabiliana na matumizi ya kemikali, hasa wanawake ni pamoja na kujifungua watoto wenye ulemavu wa viungo, watoto kupata ugonjwa wa degedege na magonjwa mengine kama vile kansa ya ngozi na ugumba kwa mwanamume au mwanamke," anafafanua Mushi na kubainisha madhara ya kemikali hizo yanachukua muda mrefu kugundulika.

# TTB yaweka malengo kuvutia watalii milioni 5 kwa mwaka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Masoko wa Bodi ya Utalii Tanzania Bara, Naassor Hassan, amesema wanaendelea kuhamasisha makundi mengi kutoka mataifa mbalimbali duniani kufika Tanzania, lengo ni kuinua sekta ya utalii pamoja na kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini kufikia milioni tano kwa mwaka.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Hifadhi ya Msitu wa Taifa wa Jozani Mkoa wa Kusini Unguja, baada ya kutembelea vivutio vya utalii ikiwamo hifadhi ya msitu huo.

Katika ziara hiyo aliambatana na wageni kutoka mataifa mbalimbali ambao walishiriki katika maonesho ya saba ya utalii wa mswahili yaliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Alisema ujio wa wageni hao utahamasisha kuongezeka kwa watalii kufika Tanzania kujionea vivutio mbalimbali na kuvitangaza katika mataifa yao.

Ofisa huyo alisema miongoni mwa mikakati wanayoifanya ni kurejesha umiliki wa Watanzania.

"Vivutio tulivyonavyo Tanzania ni vingi na ada kwa wenyeji zipo chini zaidi ikilinganishwa na wageni na soko la ndani la utalii ni muhimu pia ili kusaidia sekta hiyo maana kipindi cha covid-19 soko la utalii liliporomoka kwa sababu ya kutegemea watalii kutoka nje ya nchi," alisema.

Mwangalizi wa ofisi katika hifadhi hiyo, Haidar Ali Makame, alisema hifadhi hiyo ya kipekee kwa Zanzibar imechaguliwa kuwa ni miongoni mwa hifadhi hai kwa sababu kuna viumbe hai vya bayoanuai vinavyopatikana katika hifadhi hiyo pekee ikiwamo kima punju.

Alisema msitu huo unavivutio tofauti ikiwamo miti, wanyama, hifadhi ya mikoko na ndege ikiwamo bundi ambaye ni kivutio kikubwa cha utalii licha ya jamii kuwa na mtazamo hasi juu ya ndege huyo ambapo humshirikisha na imani za kishirikina.

Alisema mwitiko wa wageni wakiwamo wenyeji wa kutembelea hifadhi hiyo na kujifunza mambo mbalimbali ni mzuri na wanapokea wageni kupata elimu ya uhifadhi wa mazingira wakiwamo watalii na wastani kwa mwezi hupokea watalii 600.

Alisema msitu huo umezungukwa na vijiji tisa na wakiwahamasisha wanajamii kulinda na kuuhifadhi msitu huo ili kuachana na shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho ili kurithi hifadhi hiyo.

Hilaria Primapuspita kutoka Indonesia ni miongoni mwa wageni walioshiriki maonyesho ya Swahili International Tourism Export, alisema amefurahia kupata nafasi ya kufika Zanzibar ambayo ni mara yake ya kwanza na amejifunza vitu vingi.

Alisema amejionea vivutio mbalimbali vya utalii vikiwamo, kima punju wanaopatikana katika Msitu wa Hifadhi Jozani, samaki aina ya pomboo wanaopatikana katika Bahari ya Hindi Kijiji cha Kizimkazi pamoja na Mji Mkongwe ambao ni urithi wa duniani.



Mwongoza watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Jozani (kulia), akionyesha watalii kiumbehai, walipotembelea hifadhini humo, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Dk. Mwinyi: Zanzibar, Oman kuendeleza ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na Serikali ya Oman ili kudumisha ushirikiano wa historia uliopo baina ya pande mbili hizo.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na ujumbe kutoka Makumbusho ya Taifa ya Oman.

Alisema, Zanzibar na Oman bado zina uhusiano na ushirikiano wa karibu zaidi kutokana na historia za pande mbili hizo, ikiwamo historia, mila na tamaduni zao.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mtendaji Mkuu kutoka Makumbusho ya Taifa ya Oman, Jamal Al Moosawi, alisema Makumbusho ya Taifa ya Oman ni taasisi ya serikali yenye jukumu la kutunza kumbukumbu za kimkakati za taifa la nchi hiyo kwa muktadha wa kutunza kumbukumbu za diplomasia, urithi wa utamaduni wa nchi hiyo, kuhifadhi masuala ya usalama.

Alisema utamaduni wa kidiplomasia ni eneo muhimu linalotunzwa zaidi, kusema kuwa makumbusho hiyo ni taasisi pekee inayotunza kumbukumbu za migogoro ya mataifa ya kiarabu ikiwemo Syria, Mogadishu na Somalia.

Naye Waziri wa Utamaduni na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhamed, alisema ushirikiano baina ya Oman na Zanzibar umeendelea kuacha athari kubwa kwa pande mbili hizo ikiwamo mfanano wa mitindo ya tamaduni za maisha, vyakula na ustaarabu.

Ujumbe huo wa Makumbusho ya Taifa ya Oman uliongozwa na Mtendaji Mkuu, Jamal Al Moosawi, awali ulitembelea Makumbusho ya Kunduchi, jijini Dar es Salaam ambako imehifadhi magofu ya kale ikiwamo makaburi ya masultani na msikiti uliotumika tangu karne ya 15 hapa nchini.

Ujumbe huo pia uliambatana na Mkurugenzi wa Idara ya Mashariki ya Kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Abdalla Kilima na Balozi wa Mdogo wa Oman Zanzibar, Said Salim Al Sinawi.

# Zanzibar yakabiliwa na athari za mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema Zanzibar inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, kwamba njia za kukabiliana na tatizo hilo ni kulinda na kutunza vyanzo vya majisafi na kuepuka athari za mazingira.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, wakati akifungua maonesho ya chakula huko Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba ambayo yamebeba ujumbe wa "maji ni uhai na chakula kwa hivyo tutunze vyanzo vyake kwa uhai wa binadamu".

Alisema juhudi zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika upatikanaji wa huduma hiyo kwa ajili ya maisha ya binadamu na viumbe vyake ikiwamo wanyama.

Othman alisema uzalishaji wa maji umefikia asilimia 67 katika mwaka 2023 kutoka asilimia 56 mwaka 2022, huku matarajio zaidi ni kufikia asilimia 75.

Hata hivyo alisema juhudi hizo zinarudishwa nyuma na kuwapo kwa mabadiliko ya tabia ya nchi yanayoikabili dunia kwa sasa pamoja na vitendo vya kibinadamu vya uharibifu wa vyanzo vya maji ikiwamo ujenzi wa nyumba za kudumu za kuishi karibu na vyanzo hivyo.

Alisema baadhi ya vyanzo vya majisafi na salama vimeanza kukauka kufuatia tabia ya binadamu ya ujenzi wa nyumba za kudumu karibu na vyanzo hivyo.

Aidha, alisema serikali imejipanga kuimarisha kilimo cha umwagiliaji majisafi mashambani pamoja na kilimo hai cha mboga ambacho msingi wake mkubwa ni upatikanaji wa uhakika wa huduma ya maji safi na salama.

Naye Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamatta Shaame Khamis, alisema lengo la maonesho hayo ni kuhimiza mapinduzi katika sekta ya kilimo, kwa kuelimishana mbinu bora za kilimo, ufugaji na uhifadhi wa misitu, pamoja na mazao yake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Seif Shaaban Mwinyi, alisema wakulima wameshukuru hatua ya serikali kuunga mkono juhudi zao sambamba na hatua ya Rais Dk. Mwinyi kufanikisha sehemu kubwa ya gharama za maandalizi ya maadhimisho na maonyesho hayo, yanayogharimu Sh.milioni 280 kwa kila mwaka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 26 YA 2022**
**ATTORNEY GENERAL NA WENZAKE 2........WADAI**
**DHIDI YA**
**MILAGA HAMKA NA WENZAKE 40...............WADAIWA**

KWA:
HILIWI JILALA
PILI MWASHULI
NDELE MANDE
MUSA MANDE
HOLO TUNGU
SENHA DIBULU
MACHIA DIBULU
MPEMBA MOTTO
MAGANGA MOTTO
LUHENGE MOTTO
JITIMA NDUBILU
MADUKA MUNGO NG'WANABEMBE
KITINYA MATONANGE
NGASA MOTO
JUMA PELEPELE
MWANAKUNDI UDULA GELEGELE

**POPOTE MLIPO – TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamriwa na mahakama hii, kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 09/11/2023 siku ya alhamis saa 3:00 kamili asubuhi bila kukosa.
**ELEWENI KWAMBA,** mkikosa kufika siku hiyo, shauri litasikilizwa bila ninyi kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama leo hii tarehe **10/10/2023**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHAYO LOMAYANI KIPUY**
anatangaza kupotelewa na k
ya gari yenye namba za usaj
**T 562 AEV – TOYOTA CHASE**
yenye Chassis **No.**
**GX903031743.** Engine No.
**IGFE571046.** Yeyote
atakayeiona atoe taarifa kitu
chochote cha Polisi kilichop
karibu. Taarifa ya Polisi:
**PHQ/ARU/ARU/4182/2023**

## CHETI KIMEPOTEA



**ANNASTAZIA MPIGA MATHIAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S4110-0003** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BISHOP NKOLA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/18702/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Muleba, Kituo cha Muleba Mjini Mkoa wa Kagera**

**Shauri la Madai Na. 80/2023**

**Jina la Mdai .............................................GILBERT KAROLI**

**Jina la Mdaiwa ........................PHILIPO PASCHAL KAKURU**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa PHILIPO PASCHAL KAKURU wa Kalenge Kijiji Nyamigele – Biharamulo.**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta wameleta madai yake/ yao ya fedha Tshs. 16,000,000, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 27 Mwezi 10 Mwaka 2023 saa 8:30 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo, kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili, lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kukwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 10 Mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FORTUNATA LUCAS KANYEMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA WISH** yenye usajili namba **T 847 DJW.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/15331/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 104 YA 2023**
**ELINA A.MARUMA ...............MLETA MAOMBI**
**JOYCE A MARUMA..................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**IDRISA SHABANI MNYAWALE,KURWA JUMA MGOGO,FURAHA EMILY MALYA,HASSAN MTINDA HUSSEIN,SAMSON CLUONGI MAKORI,GRACE B.MASSAWE .....WAJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**GRACE B.MASSAWE**
Popote Ulipo Unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 25/10/2023 mbele ya Mwenyekiti E.MOGASA wewe mwenyewe binafsi au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 26 mwezi September, 2023.

E. MOGASA
MWENYEKITI

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 81 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late of the late EMMANUEL ERNEST LENJILA of Chamwino within Dodoma City**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**JOSEPH MKUNJILA**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 09,2023
Dated at Dodoma this 30 Day of 08, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VERNON LEO BOSCO FERNANDES** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye umiliki wa jina la **WORLD AGAPE MINISTRIES.** Namba yake ya usajili ni **T 907 AEG, TOYOTA HILUX D/CABIN.** CHASSIS NAMBA: **LN650070188.** ENGINE NAMBA **2L1513570.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/24508/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZINIA**
**Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na. 69/2023**
**JINA LA MDAI.........................LUSINDE MALUGU**
**JINA LA MDAIWA..................FURAHA HAMISI GALYA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA; FURAHA HAMISI GALYA**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA.**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 25/10/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 Mwezi 10 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE



**CHRISTOPHER JOHN REUBEN,** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S2894/0074/2019** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAKOLE SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2019. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi **PHQ/IRI/IRI/1/2023**.

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.96 OF 2023**
**IN the Matter of the late NORBERT YOHANA TINDA**

**By 1. LUCY ALOYCE MNUNGA**
**2..................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 17/10/2023.
**Dated at Morogoro this 02day of 10/ 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

JAMES JAMES anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LAND CRUISER yenye usajili namba T 955 ACN , CHASSIS NAMBA: UZJ1000129385 na ENGINE NAMBA: 2UZ9011027. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/482522/2022

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@ GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MWANZA**

**KESI YA MAOMBI MADOGO YA MADAI NAMBA 65 YA 2022**

**1. FERDINAND DEUS MTESIGWA.......................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **CATA MINING COMPANY LIMITED**
2. **SELEMANI MOHAMED KHAMESE**
3. **TANGANYIKA COMPANY LIMITED**
4. **MAHUZA MUMANGI NYAKIRANG'ANI......WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA:** SELEMANI MOHAMED KHAMESE, TANGANYIKA COMPANY LIMITED, MAHUZA MUMANGI NYAKIRANG'ANI
SHAURI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 17/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI MBELE YA MAHAKAMA HII, KWA HIVYO MNATAKIWA KUSIKILIZA SHAURI LILILOTAJWA HAPO JUU LILILOFUNGULIWA NA MDAI DHIDI YENU.
KAA- MKIJUA KUSHINDWA KUFIKA MAHAKAMA ITASIKILIZA SHAURI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA NYINYI KUWEPO.
IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 14/09/2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA.

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
**THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Tetemeko la pili laua 1000 Afghanistan

**KABUL,** Afghanistan

TETEMEKO lingine la ardhi limetikisa Magharibi mwa Afghanistan jana siku chache baada ya matetemeko mawili makubwa kutokea katika eneo hilo na kuua zaidi watu 1,000.

Kulingana na kipimo tetemeko hilo jipya lilikuwa 6.3 na lilitokea mwendo wa saa 11.10 kilomita 28 kaskazini mwa jiji la Herat.

Zaidi ya watu 100 wamejeruhiwa na kupelekwa hospitalini, maafisa wa afya walisema.

Kuna athari kubwa iliyosababishwa na tetemeko hilo, lakini bado haijabainika watu kiwango chake halisi.

Mashirika ya misaada yalisema kuna uhaba wa blanketi, chakula na vifaa vingine.

Mtu aliyeshuhudia athari za tetemeke eneo la kati la Herat, ambako baadhi ya nyumba hazijaporomoka alisema wakati wa tukio hilo aliamka na kupiga kelele huku akikimbia nje ya nyumba yake.

"Nilikuwa katika usingizi mzito kwa sababu sikuwa nimelala siku zilizopita," aliambia BBC.

"Sijawahi kuhisi karibu na kifo kama ilivyokuwa sasa," alisema. **BBC**

## Kanali Goita, Putin wateta

**BAMAKO,** Mali

RAIS wa mpito wa Mali, Kanali Assimi Goita amezungumza na Rais wa Russia Vladimir Putin na kujadili ushirikiano wa kiuchumi na kiusalama wa pande zote mbili.

Katika mazungumzo kwa njia ya simu viongozi hao walikubaliana kuimarisha uhusiano wa nchi hizo.

"Wakati wa majadiliano ya simu, nilizungumza na Rais Putin kuhusu ushirikiano wetu katika nyanja za kiuchumi, usalama na kukabiliana na ugaidi. Nilitoa shukrani zangu kwa msaada wote ambao Russia inaipa Mali," alisema Kanali Goita katika taarifa iliyochapishwa kwenye mtandao wa X.

Kauli hiyo imeungwa mkono na Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia.

Katika taarifa yake kwenye Telegram, wizara hiyo ilisema viongozi hao wawili walithibitisha dhamira yao ya pamoja ya kuimarisha zaidi uhusiano wa kibiashara na kiuchumi, ushirikiano katika kutoa usalama, na kupambana na ugaidi.

Taarifa hiyo ilieleza Mali ilitoa shukrani zake kwa misaada mbalimbali inayotolewa na Russia.

Mazungumzo hayo ni ya tatu kufanyika kwa njia ya simu kati ya viongozi hao wawili katika muda wa miezi kadhaa. **BBC**

## Gavana Burundi atupwa mahabusu

**BUJUMBURA,** Burundi

GAVANA wa Benki Kuu ya Burundi ambaye alitimuliwa kazi wiki iliyopita amekamatwa kwa tuhuma za ufisadi.

Wizara ya Sheria inamtuhumu gavana guyo, Dieudonné Murengerantwari kwa uzembe na kuhujumu uchumi wa taifa hilo, ufisadi, ufujaji wa pesa na ufujaji wa mali ya umma.

Hata hivyo, Murengerantwari hajajibu tuhumu hizo mpaka sasa.

Jumapili, Rais wa Burundi Évariste Ndayishimiye alimfukuza kazi Murengerantwari na nafasi yake kuchukuliwa na Édouard Normand Bigendako.

Murengerantwari aliteuliwa kuongoza benki kuu ya nchi hiyo miaka mitano kuanzia Agosti mwaka jana, lakini ndani ya mwaka mmoja ameondolewa madarakani.

Mwanasheria Mkuu Leonard Manirakiza, alisema kuwa madai dhidi ya gavana huyo ni ya muda mrefu na uchunguzi dhidi yake unaendelea. **BBC**



Anga la mji wa Gaza likitawaliwa na wingu zito la moshi wenye moto baaada ya ndege za Israel kuendelea kushambuliwa kwa siku tano mfululizo. **PICHA: REUITERS**

## Israel yaendelea kuiteketeza Gaza

**TEL AVIV,** Israel

ISRAEL imeendelea kufanya mashambulizi dhidi ya wapiganaji wa Hamas ukanda wa Gaza kwa siku ya tano mfululizo baada ya waziri mkuu wa nchi hiyo Benjamin Netanyahu kutangaza vita dhidi ya kundi hilo linalotawala ukanda huo.

Mashambulizi hayo ya Israel yanafuatia mashambulizi makubwa yaliyofanywa na vuguvugu la Hamas ndani ya Israel mwishoni mwa juma.

Mapigano hayo yamesababisha mashirika ya kiutu yakitafuta njia za kuwasaidia raia waliokwama katika vita hivyo.

Makabiliano ya risasi kati ya vikosi vya Israel na wanamgambo wa Palestina yamesababisha vifo vya wanamgambo watatu katika mji wa Ashkelon kusini mwa Israel.

Jeshi la Israel limesema wanajeshi wake wakisaidiwa na helikopta na ndege zinaondeshwa bila rubani wamefyatuliana risasi na magaidi kadhaa katika eneo la viwanda la Ashkelon, kilomita kadhaa Kaskazini mwa Ukanda wa Gaza, huku wakiendelea kuwatafuta wapiganaji wa kundi la Hamas waliojificha.

Jeshi la Israel pia lilisema kuwa ndege ya kwanza iliyobeba silaha za Marekani imetua nchini humo baada ya Marekani kusema itatuma mahitaji mapya ya ulinzi wa anga, risasi na msaada mwingine wa kiusalama kwa mshirika wake dhidi ya wanamgambo wa Kipalestina.

Mpaka jana asubuhi jeshi la nchi hiyo lilisema walikuwa wamefikia maeneo 450 yaliyolengwa katika muda wa saa 24.

Ilisema wanajeshi wameanza wanatumia roketi kwa mashambulizi ya ardhini.

Msemaji wa jeshi, Daniel Hagari alisema ilikuwa ni mara ya kwanza kutumia aina hii ya silaha ya kurusha risasi dhidi ya maeneo ya ndani ya Gaza tangu mzozo huo uanze 2006.

Katika hatua nyingine, ndege ya kwanza iliyobeba zana za kijeshi za Marekani imewasili katika Kambi ya Nevatim kusini mwa Israel.

"Ushirikiano kati ya wanajeshi wetu ni sehemu muhimu ya kuhakikisha usalama wa kikanda na utulivu wakati wa vita," lilisema jeshi la Israeli katika taarifa iliyochapishwa kwenye mitandao ya kijamii.

Kundi la washambuliaji kutoka kikosi cha USS Gerald R Ford pia limewasili Mashariki mwa Mediterania. **DW**

## CRDB yashiriki Mkutano Benki ya Dunia kimkakati

**MARRAKECH,** Morocco

BENKI ya CRDB imeshiriki Mkutano wa Mwaka wa Benki ya Dunia 2023, ikisisitiza dhamira yake ya kushiriki kuendeleza mchango katika maendeleo endelevu Tanzania na kuhimiza ushirikiano wa kimataifa wa kifedha.

Mada kuu ya mkutano wa mwaka huu inalenga kutokomeza umaskini kwa njia endelevu na kukabiliana na changamoto za kimataifa kupitia masuluhisho ya kibunifu, jambo linalotiliwa mkazo na Benki ya CRDB.

Benki inachangia kikamilifu katika mijadala inayolenga kuimarisha upatikanaji ajira, kuimarisha miundombinu ya kidijitali na kushiriki katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa katika mataifa yanayoendelea.

Katika mjadala unaohusu nafasi ya Sekta ya Fedha katika kuondoa umaskini na changamoto zinginezo duniani, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisisitiza mkakati wa benki hiyo kuwezesha biashara ndogo na za kati Tanzania.

Alibainisha kuwa sekta hiyo ndogo inajumuisha biashara milioni 3.2, ikichangia asilimia 27 katika Pato la Taifa na ni kusaidia maisha ya watu zaidi ya milioni tano.

"Katika uchumi wa Tanzania, biashara ndogo na za kati, ni kama mfumo wa damu, zinakuza uchumi, kutengeneza ajira na kujenga uhimilivu. Ili kuchangia uchumi na kuondoa umaskini, uwekezaji wetu katika biashara hizi ni uti wa mgongo kwa uchumi wa taifa. Benki ya CRDB inajivunia kwa kuwa mstari wa mbele katika safari ya mabadiliko, kuwezesha uendelevu wa wajasiriamali hawa, hivyo kuchangia mafanikio ya uchumi wa Tanzania," Nsekela alisema.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, benki imetoa zaidi ya Sh. trilioni 3.4 kuwezesha kundi hilo la wafanyabiashara wadogo na wa kati 50,000.

# CHE MALONE AITABIRIA SIMBA MAKUBWA CAF

**Na Saada Akida**

BEKI wa Simba, Fondoh Che Malone amesema kazi kubwa iliyoleta nchini ni kuwapa furaha mashabiki na wanachama wa timu hiyo kwa kupambana na kusaka matokeo mazuri katika kila mechi watakayocheza.

**Che Malone aliyesajiliwa Simba msimu huu kwa mkataba wa miaka miwili amekuwa msaada mkubwa katika eneo la ulinzi akichukuwa nafasi ya Mkenya Joash Onyango ambaye ametimkia Singida Fountain Gate FC.**

Akizungumza na Nipashe jana, Che Malone alisema kazi yake kubwa ni kuonyesha ushirikiano mzuri na wachezaji wenzake kwa kucheza katika kiwango bora ambacho kitawaka matokeo mazuri na hatimaye kufikia malengo yanayotarajiwa na klabu hiyo.

Beki huyo alisema anaamini wakipambana katika kila mchezo ulioko mbele yao, basi watajiweka kwenye nafasi nzuri ya kufikia malengo katika kutwaa mataji ya mashindano ya ndani na michuano ya kimataifa wanayoshiriki.

"Kazi yangu ni kucheza na kuhakikisha tunashirikiana vizuri na wenzangu kupata matokeo bora katika kila mechi tunazocheza na kufikia malengo yetu, jukumu langu ni kuhakikisha tunaendelea kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema beki huyo.

Aliongeza anaimani kubwa ya kufanya vizuri katika mechi dhidi ya Al Ahly kutoka Misri kwa kuanza vyema michuano ya Africa Football League (AFL).

Simba ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa mkononi na pointi 15 baada ya kushinda michezo yote mitano yaliyochezwa wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 13 huku mabingwa watetezi, Yanga wakiwa katika nafasi ya tatu na pointi zao 12 kibindoni.

Mbali na Ligi Kuu Bara, Wekundu wa Msimbazi pamoja na Yanga wametinga hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakiwa ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye michuano ya kimataifa.



# *Ibra Class: Nitamchapa Mchina*

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Ibrahim Mgenda 'Ibrahim Class' ameingia kambini rasmi ili kujiandaa na pambano dhidi ya Xion Tau Su kutoka China litakalofanyika Oktoba 28, mwaka huu kwenye Ukumbi wa PST Sabasaba, Dar es Salaam.

Ibrahim Class na Su watacheza pambano la raundi 10 lakini lisilo la ubingwa wakiwasindikiza Fadhili Majiha atakayepigana na Mahlangu kutoka Afrika Kusini ambao watawania mkanda wa WBC.

Akizungumza na Nipashe jana, Ibrahim Class alisema anaendelea vyema na maandalizi yake kuelekea pambano hilo ambalo anatarajia litakuwa nzuri na lenye ushindani kutokana na ubora wa mpinzani wake.

"Nimeingia kambini mapema kwa sababu ya uzito wa pambano ambalo naenda kucheza lakini pia mpinzani ninayekutana naye sio wa kumbeza natakiwa kujiandaa vizuri zaidi," alisema Ibrahim Class.

Mratibu wa matukio na habari wa Kampuni ya HB Sadc Boxing, Abdallah Neneko alisema taratibu zote muhimu zimekamilika na wanatarajia wadau wa ngumi watapata burudani safi.

Neneko alitaja mapambano mengine yatakayochezwa siku hiyo itakuwa ni kati ya bondia Nassib Ramadhani dhidi ya Zolisa Batyi kutoka Afrika Kusini wakati Spumoni Muki ataonyesha ubabe na Loveleen Thaakur wa India.

" Kupitia kampuni yetu Watanzania wategemee mapambano mazuri na watashuhudia mabondia wenye viwango wakija kupigana nchini," alisema Neneko.



Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kigamboni wakicheza muziki katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Wazee iliyofanyika kwenye Viwanja vya Mji Mwema, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# New City yazinduka Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya New City FC imepata ushindi wa kwanza msimu huu baada ya kuifunga Jamhuri mabao 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uwanja wa Finya juzi.

Kufuatia ushindi huo, New City imefikisha pointi tano na kupanda hadi nafasi ya 11 katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Razak Salum alisema haikuwa kazi rahisi kwa wachezaji wake ambao wamevuna pointi nne nne katika michezo miwili ya ugenini.

Salum alisema ushindi huo umetokana na wachezaji wake kupambana na kuhakikisha wanashinda kila mechi kwa kucheza kwa kujitolea.

New City FC itashuka tena dimbani Oktoba 21, mwaka huu kucheza dhidi ya mabingwa watetezi, KMKM.

Ligi hiyo itaendelea tena leo kwa Kipanga FC kuvaana na Ngome Fc kwenye Uwanja wa Mau kuanzia saa 10:15 jioni.

# Bodi ya Ligi yafurahishwa na ushindani

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu (TPLB), imesema imeridishwa na mwenendo wa ligi hiyo ambayo sasa iko katika raundi ya tano na imesimama tena kupisha kalenda ya FIFA, imeelezwa.

Ofisa Habari wa bodi hiyo, Karim Boimanda, amesema Ligi Kuu imekuwa na mvuto na ushindani mkubwa zaidi kuliko msimu uliopita.

Boimanda alisema pia viwango vya waamuzi wanaochezesha vimeongezeka ingawa imekiri kuna changamoto kwa baadhi yao, hivyo wataendelea kutoa semina kwa ajili ya kuboresha viwango vyao.

"Kwa tathmini ya haraka haraka mpaka kufikia raundi ya tano Ligi Kuu imekuwa ni mizunguko bora inayotupa ishara ya namna msimu huu 2023/24 utakavyokuwa, levo ya ushindani imekuwa kubwa sana kuliko tulivyotarajiwa, kwa hakika kabisa ukitazama michezo ambayo imefanyika, unaweza ukaona wazi kwa nini ligi hii inaimbwa na inaendelea kutangazika hapa barani Afrika," alisema Boimanda.

Aliongeza changamoto zilizotokea zitafanyiwa kazi na alifungua kutegemea jicho la mwamuzi pekee si kitu rahisi sana na ndio sababu Ulaya walishaondoka na kuhamia katika matumizi ya VAR.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY KUMBAKIZA HAALAND

KLABU ya Manchester City imeonyesha nia ya kumpa mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23 mkataba mpya ambao utaondoa kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 173. ***(Gazzetta dello Sport)***

### INACIO ATAJWA UNITED

MANCHESTER United imemwongeza mlinzi wa Sporting Lisbon na Ureno, Goncalo Inacio mwenye umri wa miaka 22 katika orodha ya wachezaji wanaolengwa huku wakipania kuimarisha safu yao ya ulinzi msimu ujao. ***(Mirror)***

### PHILLIPS KUONDOKA CITY

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kalvin Phillips anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo Januari, huku Newcastle United na Everton zikiwa miongoni mwa wanaomtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 27. ***(Mail)***

### TONEY ANUKIA ARSENAL

ARSENAL ipo katika mikakati ya kumsajili mshambuliaji wa England, Ivan Toney kutoka Brentford na mazungumzo yamefanyika kati ya klabu hizo mbili, huku Chelsea pia wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(TeamTalks)***

### MASON KUITWA JAMAICA

JAMAICA inaweza kumpa mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu ya Getafe ya Hispania fursa ya kurejea katika soka la kimataifa - miaka mitatu baada ya kucheza soka la juu nchini England. ***(Mirror)***

### GITTENS KUTUA ARSENAL

ARSENAL inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua winga wa Borussia Dortmund na na Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 19, Jamie Bynoe-Gittens. ***(Bild)***

### KIMMICH ANUKIA CITY

MANCHESTER City inavutiwa na kiungo wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich na Bayern Munich huenda wakalazimika kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ikiwa hataongeza mkataba wake zaidi ya mwaka 2025. ***(90 Min)***

### JUVE YAMTAKA SANCHO

WINGA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 yuko tayari kuhama ifikapo Januari huku Juventus na Borussia Dortmund zikivutiwa na nyota huyo. ***(Mail)***

### BROJA AINGIA SOKONI

INTER Milan imekataa uhamisho wa Januari wa kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 22. ***(Fabrizio Romano)***

### CONTE KUMRITHI GARCIA

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Antonio Conte yuko tayari kutua Napoli ikiwa mabingwa hao wa Serie A watafanya uamuzi wa kumfukuza. Rudi Garcia. ***(Calciomercato)***

## DONDOO KA
## MAGAZETI YA




# MADRID YAFUNGUKA USAJILI WA MBAPPE

**MADRID,** Hispania

**●●● Vigogo hao wanaamini mchakato wa kumnasa mshambuliaji huyo...**

BOSI wa Real Madrid, Jose Manuel Otero Lastre amefunguka kuhusu mipango ya klabu hiyo kumsajili mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe ifikapo mwaka 2024.

**Kwa muda mrefu nyota huyo amekaa kileleni mwa orodha ya wachezaji wanaotamaniwa Madrid na vigogo hao wa Hispania wanaamini watapata saini ya Mbappe kwa uhamisho wa bure msimu ujao wa joto wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika.**

Huku kukiwa na hofu anaweza kuondoka bure, PSG walimweka Mbappe auzwe wakati wa majira ya joto lakini hakuna ofa rasmi kutoka kwa Madrid iliyowahi kutolewa.

90min iliripotiwa wakati huo, wasiwasi juu ya bei yake ilisababisha Madrid kuelekeza juhudi zao katika uhamishaji wa bure mwaka 2024.

Akijibu maswali kupitia chaneli ya Remontada Blanca Twitch, Otero ambaye amefanya kazi pamoja na Rais, Florentino Perez tangu mwaka 2002 - alijibu maswali mengi kuhusu mipango ya Madrid kwa Mbappe.

"Mbappe alikuwa na hakuwa na fursa ya kusajiliwa na Real Madrid msimu huu," alisema Otero.

"Ili kuja, angelazimika kuacha mafao ya juu sana ambayo tayari alikuwa amekubaliana na Paris Saint-Germain. Zaidi ya hayo, kulikuwa na ada ya kuhamisha kulipa.

"Kiasi ambacho kingelipwa ili kumsajili Mbappe mwaka mmoja uliopita kilikuwa cha kichaa. Haikuwa na maana kumsajili Mbappe mwaka mmoja kabla, ingawa Madrid walivunjwa katika nafasi ya Karim Benzema."

Aliendelea: "Tunamatumaini Mbappe ana mawazo sawa na (Jude) Bellingham. Ninaamini atakuja. Mbappe atapata utukufu atakapokuja Real Madrid. Atashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya siku moja.

"Sasa inaonekana PSG hawana nguvu zaidi kuliko hapo awali kwa sababu hawana tena wachezaji wazuri kiasi hicho. Madrid inawahakikishia usalama, umakini unaoleta matokeo. Ninaamini atasema ndiyo wakati yeye ni mchezaji huru. Mbappe alizaliwa kuichezea timu kama Real Madrid."

Hii si mara ya kwanza kwa Madrid kutafuta saini ya Mbappe kwa uhamisho wa bure. Mfaransa huyo alikaribia kujiunga nao mnamo 2022 kabla ya kusaini nyongeza ya mkataba ya kushtukiza.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,161,7

MECHI KALI
SPAIN
VERSUS
SCOTLAND
1 | 1.29
X | 5.28
2 | 10.56

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAGUIRE: BECKHAM ALINIPA UJASIRI




**LONDON,** England

HARRY Maguire amefichua jinsi simu kutoka kwa David Beckham ilimsaidia kukabiliana na unyanyasaji kutoka kwa mashabiki, ambao wakati fulani umekuwa mbaya sana na familia yake ilikaa mbali na michezo.

Mchezaji huyo alistahimili usiku wa kustaajabisha kama mbadala wa kipindi cha pili katika ushindi wa 3-1 wa England dhidi ya Scotland mwezi uliopita, akishangiliwa na maelfu ya mashabiki wa nyumbani kabla ya kila mguso wake kukejeliwa ikiwamo bao la kujifunga la dakika ya 67.

Hapo awali Maguire alilengwa na mashabiki wa Arsenal wakati akiwakilisha Manchester United kwenye Uwanja wa Emirates na beki huyo wa kati amekabiliwa na shutuma nyingi kwenye mitandao ya kijamii baada ya kukosa nafasi chini ya Erik ten Hag pale Old Trafford.

Kocha wa England, Gareth Southgate alidai baada ya mechi ya Scotland "sijawahi kujua mchezaji anatendewa namna hii" na Maguire akafichua Beckham alimpigia simu siku chache baada ya mchezo huo na kumpa sapoti.

Beckham alivumilia hasira kali kutoka kwa mashabiki wa England waliokasirishwa na kadi nyekundu katika mechi ya mwaka 1998 ya Kombe la Dunia walipofungwa na Argentina.

Akizungumzia simu kutoka kwa Beckham, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 48, Maguire alisema: "Ilimaanisha kila kitu. Nimezungumza katika maisha yangu yote kuhusu David Beckham kuwa mtu niliyemtazama na kumtazama nilipokuwa mvulana mdogo.



## Neville aiondoa United 5 bora

**MANCHESTER,** England

GARY Neville haamini Manchester United itamaliza katika nafasi tano bora za juu kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Mashetani Wekundu hao wamekuwa na mwanzo mgumu wa msimu, wakipoteza michezo sita kati ya 11 katika mashindano yote chini ya kocha Erik ten Hag.

Beki wa zamani wa klabu hiyo, Neville anadhani kuna matatizo makubwa katika kikosi cha United na haoni uwezekano wa kumalizika kwenye tano bora.

Akizungumza kwenye Podcast ya Gary Neville alisema: "Sidhani Manchester United itamaliza katika nafasi tano za juu msimu huu.

"Chelsea haiko mbali kama watapata mshambuliaji wa kati na kiungo wa kati. Ingawa wametumia pauni bilioni moja bado wanahitaji wachezaji wawili.

Neville pia aliangazia uchezaji usiolingana wa mchezaji aliyesajiliwa kipindi cha majira ya joto, Andre Onana.

"Ikiwa golikipa wako hajatulia na kuna ukosefu wa utulivu katika hilo, inaleta tatizo kubwa. Na ndio tatizo kubwa la United."

## HABARI MICHEZO

95,478/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/10/23 | 19:30 | Sporting Gijon vs Real Zaragoza | 2.12 | 3.00 | 3.65 |
| 02. 14/10/23 | 19:30 | FC Cartagena vs Racing Santander | 2.24 | 3.05 | 3.25 |
| 03. 14/10/23 | 21:45 | Hungary vs Serbia | 2.42 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 14/10/23 | 23:00 | Ituano vs CR Brasil | 2.30 | 2.95 | 3.25 |
| 05. 14/10/23 | 23:00 | Detroit City vs Pittsburgh Riverhounds | 2.65 | 3.40 | 2.25 |
| 06. 15/10/23 | 00:00 | Deportivo Pereira vs La Equidad | 2.15 | 3.05 | 3.05 |
| 07. 15/10/23 | 02:05 | Alebrijes de Oaxaca vs Cancun | 2.21 | 3.20 | 2.85 |
| 08. 15/10/23 | 02:10 | Atletico Nacional vs Independiente Medellin | 2.13 | 3.10 | 3.05 |
| 09. 15/10/23 | 03:00 | Cuiaba vs Cruzeiro | 2.35 | 3.05 | 3.05 |
| 10. 15/10/23 | 05:00 | Monterey Bay vs Orange County | 2.16 | 3.40 | 2.75 |
| 11. 15/10/23 | 05:30 | Las Vegas Lights vs San Diego Loyal | 2.85 | 3.40 | 2.11 |
| 12. 15/10/23 | 05:30 | LA Galaxy vs Real Salt Lake | 2.25 | 3.65 | 2.50 |
| 13. 15/10/23 | 08:00 | Osaka vs Gifu | 2.75 | 2.90 | 2.43 |
| 14. 15/10/23 | 17:15 | Eldense vs Elche | 3.30 | 3.05 | 2.22 |
| 15. 15/10/23 | 17:30 | Preussen Munster vs 1860 Munich | 2.17 | 3.35 | 2.75 |
| 16. 15/10/23 | 21:30 | CA Estudiantes vs Tristan Suarez | 2.20 | 3.30 | 3.10 |
| 17. 15/10/23 | 21:45 | Ponte Preta vs AC Goianiense | 3.10 | 2.90 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 12/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2358 | Pazarspor vs Silifke Belediyespor | 2.27 | 3.25 | 2.84 |
| 13:00 | 4282 | Malaga vs Melilla | 1.34 | 4.19 | 8.78 |
| 13:00 | 4845 | CD Cortes vs CD Sauzal | 1.85 | 3.47 | 3.88 |
| 13:00 | 5843 | Adiyaman 1954 SK vs Viven Bornova FK | 2.19 | 3.45 | 2.70 |
| 14:00 | 2347 | Maldives vs Bangladesh | 2.12 | 3.16 | 3.21 |
| 14:00 | 3801 | Taiwan vs Timor-Leste | 1.23 | 5.29 | 10.17 |
| 14:30 | 1480 | Singapore vs Guam | 1.08 | 7.55 | 23.46 |
| 14:45 | 5569 | Nepal vs Laos | 1.39 | 4.37 | 6.51 |
| 15:00 | 1201 | Indonesia vs Brunei Darussalam | 1.03 | 11.23 | 27.56 |
| 15:00 | 2228 | Dire Dawa Kenema FC vs Ethiopia Bunna SC | 3.16 | 3.11 | 2.17 |
| 15:00 | 2901 | Cambodia vs Pakistan | 1.70 | 3.41 | 4.58 |
| 16:30 | 1696 | Qizilqum vs Otmk Olmaliq | 2.90 | 3.15 | 2.17 |
| 17:00 | 3421 | FC Viktoria Marianske Lazne vs Viktoria Plzen | 19.32 | 9.76 | 1.06 |
| 17:00 | 4553 | Afghanistan vs Mongolia | 1.41 | 4.17 | 6.72 |
| 17:00 | 5004 | Georgia U21 vs Netherlands U21 | 4.98 | 3.97 | 1.55 |
| 17:30 | 2278 | Turegano CF vs CD Santurtzi | 2.35 | 3.50 | 2.67 |
| 18:00 | 1076 | UE Rubi vs UD Rotlet Molinar | 1.85 | 4.12 | 3.30 |
| 18:00 | 1553 | CF Tardienta vs CD Zirauki | 1.65 | 3.93 | 4.44 |
| 18:00 | 4269 | Ethiopia Nigd Bank vs Hadiya Hosahina FC | 3.10 | 3.00 | 2.25 |
| 18:30 | 3176 | CD Melilla vs Deportivo Murcia FC | 1.60 | 4.12 | 4.63 |
| 18:30 | 4137 | CD Monte vs CD Boiro | 2.48 | 3.61 | 2.48 |
| 18:30 | 5949 | CD Quintanar vs Union Zona Norte | 2.06 | 3.67 | 3.05 |
| 19:00 | 2672 | Montenegro vs Lebanon | 1.40 | 4.54 | 7.82 |
| 19:00 | 3426 | Latvia vs Armenia | 4.33 | 3.38 | 1.88 |
| 19:00 | 3534 | Russia vs Cameroon | 2.09 | 3.33 | 3.54 |
| 19:00 | 3735 | Georgia vs Thailand | 1.22 | 6.12 | 12.65 |
| 19:00 | 3884 | SD Beasain vs CD Derio | 1.35 | 4.30 | 6.80 |
| 19:00 | 4000 | United Arab Emirates vs Kuwait | 1.67 | 3.49 | 5.71 |
| 19:00 | 4173 | Israel U21 vs Estonia U21 | 1.09 | 7.52 | 21.33 |
| 19:00 | 4256 | Egypt vs Zambia | 1.65 | 3.68 | 5.47 |
| 19:00 | 4644 | Karsiyaka vs Bigaspor | 1.18 | 6.11 | 11.20 |
| 19:00 | 5053 | Atletico Arteixo vs Viveiro CF | 2.08 | 2.98 | 3.39 |
| 19:30 | 3475 | FC Bidezarra vs CD Cantolagua | 2.26 | 3.18 | 2.83 |
| 19:30 | 4400 | CP Moralo vs SP Villafranca | 1.84 | 3.25 | 3.75 |
| 20:00 | 2075 | Yemen vs SRI Lanka | 1.14 | 5.91 | 18.34 |
| 20:00 | 3074 | Sweden vs Moldova | 1.21 | 6.34 | 13.75 |
| 20:30 | 5391 | Luxembourg U21 vs Ukraine U21 | 15.26 | 6.71 | 1.13 |
| 21:30 | 2014 | Austria U21 vs Norway U21 | 1.86 | 3.46 | 3.66 |
| 21:45 | 3278 | Belarus vs Romania | 5.91 | 3.80 | 1.59 |
| 21:45 | 3552 | Andorra vs Kosovo | 8.05 | 4.24 | 1.43 |
| 21:45 | 4497 | Albania vs Czech Republic | 3.26 | 3.11 | 2.32 |
| 21:45 | 4962 | UCD Dublin vs Bohemians FC | 13.15 | 6.27 | 1.14 |
| 21:45 | 5085 | Faroe Islands vs Poland | 9.32 | 4.66 | 1.36 |
| 21:45 | 5255 | Spain vs Scotland | 1.29 | 5.28 | 10.56 |
| 21:45 | 5307 | Cyprus vs Norway | 12.72 | 5.72 | 1.24 |
| 21:45 | 5373 | Croatia vs Turkey | 1.70 | 3.60 | 5.19 |
| 21:45 | 5436 | England U21 vs Serbia U21 | 1.33 | 4.67 | 7.51 |
| 22:00 | 3461 | Sint Maarten vs Saint Kitts and Nevis | 6.30 | 4.47 | 1.39 |
| 22:00 | 5589 | Algeria vs Cape Verde | 1.49 | 4.13 | 6.77 |
| 23:30 | 4213 | Colombia vs Uruguay | 2.14 | 3.28 | 3.49 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# RC MAKALLA AWATOLEA UVIVU 'MAFAZA' PAMBA

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amewataka wachezaji wa Timu ya Pamba kuacha tabia ya kucheza kwa 'ufaza' uwanjani, badala yake wajitume na wafanye mazoezi ya ziada ili kutimiza malengo ya mkoa ya kuwa na timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Makalla alisema hayo juzi alipotembelea mazoezi ya timu hiyo jijini humo na kuonyesha kusikitishwa na matokeo ya timu hiyo hasa mechi za ugenini na kusisitiza kuwa hakuna namna ya watafikia malengo yao kama wachezaji na benchi la ufundi hawatatimiza wajibu wao kwa asilimia 100.

**"Nimeona baadhi ya mechi, kuna wachezaji 'mafaza' hapa, wanakabia macho, wanataka mpira waletewe miguuni, sisi tunawaita mabwana shamba maana kazi yao wanasimama na kugeuka tu kama wanakagua shamba, hakuna kazi wanayofanya.**

"Hapa Mwanza tulikuwa na Pamba, Toto African, Mbao FC, Alliance, zote hazipo Ligi Kuu, najiuliza kwa nini historia ya Mwanza kwenye soka inataka kupotea?", alihoji Mkuu huyo wa Mkoa aliyekuwa ameambatana na wachezaji wa zamani wa timu hiyo waliotamba miaka ya 1980 na 1990.

Alisema ili kuirudisha Mwanza kwenye ramani ya soka la Ligi Kuu ni lazima wachezaji wajitume uwanjani, makocha wafanye kazi zao kwa uhakika na viongozi pia wafanye kazi zao.

Kwa upande wake, mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo ya Yanga, Fumo Feliciane, aliwaambia wachezaji kuwa wana tatizo la kutojituma tofauti na wakati wanacheza wao.

"Ni aibu kwa kweli, leo sisi Mwanza tunabebwa na Geita Gold kutuletea mechi ili twende kutazama mpira CCM Kirumba kweli? hii ni aibu kwa Mkoa wetu ambao huko nyuma ulikuwa unaogopewa kwa kuwa na timu imara," alisema Fumo.

Timu hiyo inayocheza Ligi ya 'Champinship', iko kwenye nafasi ya saba ya msimamo, ikicheza mechi tano, ineshinda mbili, imetoka sare mbili na kupoteza moja, ikijikusanyia pointi nane.



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya U-20 (Tanzanite), Diana Mnally, akijiandaa kupiga mpira katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Djibouti iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Tanzanite imesonga mbele. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

## Simba yaishtukia Al Ahly

INATOKA UKURASA 24

yetu na sisi tumeshtukia hili, kumfunga Al Ahly si jambo geni bali tunahitaji kumtoa mpinzani wetu katika mashindano haya kwa kusaka ushindi hapa nyumbani na ugenini," alisema Ahmed na kusisitiza Wanasimba kuungana ili kufanikiwa lengo lao la kusonga mbele katika michuano hiyo.

Aliongeza kuwa maandalizi ya ndani na nje ya uwanja kuelekea kwenye mchezo huo mkubwa Afrika yanaendelea vizuri na wanapata ushirikiano mzuri kutoka kwa Serikali na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

"Hapo awali michuano hii ilijulikana kama Super League lakini sasa wanaiita Afrika Football League ambayo ni michuano mikubwa Barani Afrika na inashirikisha watu bora pekee ambao Simba ndio ni timu pekee katika ukanda huu wa soka wa Afrika Mashariki na Kati, haya mashindano hayako kwa bahati mbaya bali Simba imepambana na kuvuja jasho hadi imefika kushiriki michuano hii mikubwa."

## *Mabao 89 yatinga nyavuni Ligi Bara*

INATOKA UKURASA 24

Ngoye, ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC, JKT Tanzania iliyowekwa kimiani na Daniel Lyanga, timu yake ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Kagera Sugar, Tabora United ikitumbukizwa na Erick Okutu, akiiongoza timu yake kuifunga Dodoma Jiji mabao 2-1.

Geita Gold ilikosa penalti yake kupitia kwa Elius Maguri katika mechi ambayo timu hiyo ilipoteza mchezo kwa mabao 2-1 dhidi ya KMC.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha kalenda ya FIFA ambapo Taifa Stars inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Sudan, ambayo itachezwa Saudi Arabia.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 12, 2023

Nipashe




Neville aiondoa Utd 5 bora UKURASA 22



## Takwimu za Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya michezo mitano

- **89** - Mabao yaliyofungwa Ligi Kuu
- **62** - Idadi ya wafungaji wa mabao yote
- **40** - Idadi ya mechi zilizochezwa hadi raundi ya tano
- **30** - Idadi ya mechi zilizotoa mshindi
- **10** - Mechi zilizomaliza na matokeo ya sare
- **21** - Idadi ya mechi zilizotoa mshindi timu ikicheza nyumbani
- **9** - Mechi ambazo timu zimeshinda zikicheza ugenini
- **6** - Idadi ya penalti zilizotolewa na waamuzi hadi sasa
- **5** - Penalti zilizotumbukia wavuni
- **3** - Idadi ya mechi ambazo Simba imeshinda ugenini, Yanga na Azam zikishinda nyumbani

# MABAO 89 YATINGA NYAVUNI LIGI BARA

### ●●● Yafunika ya mechi tano msimu uliopita, Baleke aongoza, Yanga kinara nyumbani, Simba...

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya mabao 89 yamezamishwa nyavuni kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya tano kwa michezo 40 iliyochezwa mpaka sasa tofauti na msimu uliopita ambao hadi kufikia raundi hiyo makipa walishaokota mipira kimya ni mara 81 tu, ikiwa ni ongezeko la mabao manane msimu huu.

**Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo la Nipashe, kwa msimu uliopita mpaka kufikia raundi ya tano, mechi 28 zilitoa mshindi ikiwa ni pungufu ya mechi mbili msimu huu, na sare zilikuwa 12 ikiwa ni ongezeko la mechi mbili za msimu huu kwa michezo 40 iliyochezwa.**

Msimu uliopita hadi kufikia raundi ya tano, mechi 19 timu zilishinda nyumbani, pungufu ya mechi mbili msimu huu michezo 21, mara tisa timu zikishinda ugenini sawa kabisa na msimu huu, sare zikiwa 12, tofauti na 10 za msimu huu.

Penalti tano zilikuwa zimepatikana msimu uliopita hadi kufikia raundi ya tano na zote ziliwekwa wavuni, tofauti kidogo na msimu huu ambapo zimepatikana sita, tano zikifungwa na moja ikikoswa.

Kwa msimu huu mabao hayo 89 yamefungwa na jumla ya wachezaji 62 wakiongozwa na Jean Baleke wa Simba ambaye ndiye kinara mpaka sasa akipachika jumla ya mabao matano.

Kati ya mabao hayo ya msimu huu, 52 yamefungwa kwa mguu na kulia, 25 yakipachikwa kwa mguu wa kushoto na yaliyobaki ni ya kichwa.

Takwimu za Nipashe zinaonesha kuwa kati ya mechi 40 zilizochezwa, 30 zimetoa mshindi, Simba ikiwa inaongoza kwa kushinda asilimia 100 ya mechi zake tano ambazo ni nyingi kuliko timu nyingine na 10 zikiwa ni matokeo ya sare, Namungo FC ikiwa na sare nyingi kuliko timu nyingine, ikifanya hivyo mara tatu.

Kati ya mechi 30 za ushindi, mechi 21 zimetoa mshindi kwa timu zilizocheza kwenye viwanja vyake vya nyumbani, Yanga na Azam zikiongoza kwa kushinda mechi nyingi zikicheza nyumbani, kila moja ikishinda mara tatu.

Yanga ilipata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya KMC na JKT Tanzania ikitumia Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kama uwanja wake wa nyumbani, Azam ikizifunga Tabora United mabao 4-0, Prisons 3-1 na Singida Fountain Gate mabao 2-1 ikiwa nyumbani pia.

Ni mechi tisa pekee ambazo timu zimepata ushindi ugenini, Simba ikiongoza kwa kushinda mechi nyingi. Imeshinda mechi tatu ugenini dhidi ya Mtibwa Sugar mabao 4-2, Prisons mabao 3-1 na Singida Fountain Gate mabao 2-1.

Kwenye idadi hiyo ya mabao 89 ya msimu huu, matano yamefungwa kwa mikwaju ya penalti, Simba ikiongoza kwa kupata penalti mbili kati ya sita zilizotolewa mpaka sasa, moja ikiota mbawa.

Ilipata penalti kwenye mechi dhidi ya Coastal Union iliyofungwa na Baleke, Simba ikishinda mabao 3-0, na nyingine dhidi ya Prisons, Saido akiikwamisha wavuni kwenye ushindi wa mabao 3-1.

Timu zingine zilizopata penalti moja moja ni Namungo iliyofungwa na Fabrice

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yaishtukia Al Ahly

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya Simba ni kama umewashtukia wapinzani wao kwenye mashindano ya Africa Football League (AFL), Al Ahly ambao wamewazuia nyota wao kwenda kwenye majukumu ya timu zao za taifa na sasa Wekundu hao wameamua kuingia kambini leo kujiandaa na mchezo huo.

Wachezaji wa Simba awali walipewa mapumziko mafupi baada ya Ligi Kuu kusimama kupisha michezo ya kimataifa ya kalenda ya FIFA.

Uongozi wa Simba sasa umepanga kuwasiliana na mashirikisho ya soka katika nchi ambazo wachezaji wake wameitwa kwa ajili ya majukumu ya timu za taifa, kuyaomba kuwaruhusu kurejea nchini mapema kujiunga na kambi ya timu hiyo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kuwa wameamua kuchukua maamuzi hayo kutokana na umuhimu wa mchezo huo wa ufunguzi wa mashindano hayo utakaochezwa Oktoba 12 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Huu mchezo ni mkubwa, wenzetu wameamua kuwazuia wachezaji wao kwenda kujiunga na timu zao za taifa, na sisi kwa kuuchukulia kwa uzito mkubwa mchezo huu, tumeanza mchakato wa kuwasiliana na mashirikisho ya soka ambayo wachezaji wetu wameitwa kujiunga na timu zao za taifa, tutawaomba wawaachie warejee na kwa wale ambao hawajaenda wasiende ili waingia kambini kujiandaa na mchezo huu," alisema Ahmed na kuongeza,

"Hii mechi yetu itakuwa ngumu kwa sababu ya ubora wa kikosi cha wapinzani wetu, Al Ahly wanaifahamu Simba kwa sababu wamewazuia wachezaji wao kwenda kwenye majukumu ya mataifa yao kwa ajili

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002